Nipashe
Jumamosi Aprili 6, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579885
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Mbatia ataja sababu Kamati ya Bunge kuonekana ya CCM

UKURASA 4




UKURASA 13

# Bunge labariki msajili kuvishughulikia vyama

UKURASA 2


Jaji Francis Mutungi
Spika Job Ndugai

## Serikali yabanwa ukosefu wa ajira

**MBUNGE** ashangaa wahitimu vyuo kuachwa hivi hivi, ataka majibu kuhusu ahadi ya jambo hilo...

*Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MAGUFULI AMSHTUKIA MKANDARASI MZAWA**
RAIS John Magufuli ameshtukia ubadhirifu wa fedha uliofanywa na mkandarasi mzawa...

UKURASA WA 3

**UPELELEZI KESI YA DK. TENGA WAIVA**
MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeambiwa kwamba upelelezi wa kesi inayowakabili vigogo wa Kampuni ya Six Telecoms...

UKURASA WA 3

**ASHINDA KURA ZA MAONI CCM KUMRITHI NASSARI ARUMERU**
MWENYEKITI wa Umoja wa Wazazi (CCM) Mkoa wa Arusha, Dk. John Pallangyo, ameshinda...

## Kampeni ya Jokate yakusanya mil. 915/-

UKURASA 3

MICHEZO
SIMBA: NI USHINDI TU UK. 32
MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Bunge labariki Msajili kuvishughulikia vyama

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BUNGE limeitaka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuchunguza na kufuatilia mienendo ya vyama vya siasa na kuchukua hatua stahiki kwa chama kitakachovunja misingi ya katiba na sheria za nchi.

Kauli hiyo ya Bunge imetoka ikiwa ni takribani wiki tatu tangu Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa ikiandikie barua Chama cha ACT- Wazalendo kwa kushindwa kuwasilisha kwake, taarifa ya fedha zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 2013/14.

Katika barua hiyo, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa pia ilieleza kusuduo la kukifuta chama hicho kutokana na watu wanaodaiwa kuwa wanachama wake kuchoma bendera za Chama cha Wananchi (CUF) na kudaiwa kupandisha bendera ya ACT wakitamka maneno yenye kuashiria udini.

Akiwasilisha bungeni mjini Dodoma juzi taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za serikali na mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka ujao wa fedha, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Najma Murtaza Giga, alisema kamati inashauri ofisi hiyo iendelee kufuatilia mienendo ya vyama vya siasa kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na weledi.

Alisema usimamizi huo ufanyike kwa lengo la kulinda umoja, udugu, amani, ulinzi

INAENDELEA UK 8



Rais John Magufuli, akivuta utepe pamoja na Waziri wa Elimu Prof. Joyce Ndalichako kuzindua chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kilichopo wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: IKULU**

## Magufuli amshtukia mkandarasi mzawa

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli ameshtukia ubadhirifu wa fedha uliofanywa na mkandarasi mzawa aliyejenga chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (Veta) Namtumbo mkoani Ruvuma kwa gharama ya Sh. bilioni 6.4, ambaye bado hajamaliza baadhi ya kazi.

Magufuli alilazimika kumsimamisha mkandarasi huyo, baada ya kubaini kuwa majengo 11 aliyojenga katika chuo hicho, hajamaliza kupiga mbao za kingo za mabati ingawa ameshapaka rangi kuashiria kumaliza ujenzi.

Alishtukia ujanja huo jana wilayani Namtumbo katika ziara yake ya kikazi mkoani Ruvuma na kumwagiza mkandarasi huyo kuhakikisha anakamilisha kazi aliyobakisha.

"Nimefanya kazi Wizara ya Ujenzi kwa miaka mingi, sijawahi kuona mkandarasi hajamaliza kazi ya kupiga mbao za pembeni ya bati akapaka rangi. Labda mlifanya hivyo ili nije nizindue, lakini kazi haijakamilika na kama mmeambiwa imekamilika tayari wana Namtumbo mmeshapigwa," alisema.

Aliwaeleza wananchi waliohudhuria mkutano huo kuwa mkandarasi huyo amepewa Sh. bilioni 6.4 za kujenga majengo 11 ya chuo hicho, yakiwamo makubwa tisa lakini katika ukaguzi aliofanya wa haraka haraka, hajaona thamani ya fedha hizo.

"Fedha zinazotolewa na serikali zinauma kuja kujenga majengo ambayo hayana thamani. Huenda fedha hizi zingetumika kununua dawa katika hospitali mbalimbali nchini ili wagonjwa watibiwe," alisisitiza Rais Magufuli.

INAENDELEA UK 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
04/04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya kesho JUMAPILI tarehe 07/04/2019kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa Kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA ,** Gari hilo lenye namba za usajili: **T374 OLQ/T944 DPE**

2. Garihilolinavipimovifuatavyo:
**Urefu - mita 21**
**Upana - mita 3.8**
**Kimo - mita 4.9**

3. Njia itakayotumika DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA kupitia VIGWAZA.gari litasafiri muda wa mchana tu(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

215160502

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*


# Serikali yabanwa ukosefu ajira

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Aida Khenani (Chadema), ameitaka serikali kulieleza Bunge kwa nini haitoi ajira kwa vijana waliohitimu katika vyuo mbalimbali vya elimu nchini.

Akichangia bungeni mjini Dodoma jana mjadala kuhusu mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za serikali na mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka ujao wa fedha, mbunge huyo alisema tangu mwaka 2015, serikali haijatoa ajira kwa vijana waliohitimu elimu ya juu kutoka vyuo vikuu mbalimbali nchini.

Alisema nafasi za ajira zinazotolewa na serikali haziakisi na haziendani na idadi ya vijana wanaohitimu vyuo vikuu nchini kila mwaka.

"Upatikanaji wa ajira kwa vijana wanaohitimu vyuo vikuu kwa sasa ni tatizo kubwa katika nchi yetu, serikali ituleze hapa bungeni kwanini haiajiri vijana wetu. Nina ujumbe kutoka kwa vijana wengi ambao wanataka tuiulize serikali ni lini itatoa ajira kwao," mbunge huyo alisema.

Juzi jioni, akichangia mjadala huo, Mbunge wa Kuteuliwa, Anne Kilango Malecela (CCM), alisema kuna haja serikali kuweka nguvu nyingi kwenye uwekezaji, hasa katika zao la pamba.

Alisema Tanzania inashika nafasi ya 22 duniani kwa uzalishaji wa pamba, hivyo kuna haja kuwekeza katika zao hilo ikiwa ni pamoja na kujenga viwanda vipya na kufufua viwanda vya nguo vilivyopo nchini.

Baada ya mbunge huyo kuwasilisha mchango wake, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliyekuwa anaongoza kikao hicho, alisimama na kumpongeza kwa mchango wake mzuri na kuwataka wabunge wengine kuiga aina ya uchangiaji wake bungeni.

Naye Mbunge wa Kaliua, Magdalena Sakaya (CUF), mbali na kuunga mkono hoja ya Malecela kuhusu uwekezaji, aliipongeza serikali kwa kuboresha na kuimarisha huduma za kibingwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Alisema vifaa vya Sh. bilioni 12 vilivyonunuliwa na serikali kwa ajili ya JKCI vimeboresha huduma

INAENDELEA UK 8

HABARI KITAIFA

# Kampeni ya Jokate yakusanya mil. 915/-

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (pichani), amesema kampeni ya tokomeza ziro wilayani humo kwa kuchangia ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa kike, imewezesha kukusanya Sh. milioni 915 kati ya Sh. bilioni 1.3 ambazo ni asilimia 74 ya lengo.

Amesema fedha taslimu ambazo zimeshawekwa benki hadi jana ni Sh. milioni 80 na bado wameendelea kupokea ahadi za wadau mbalimbali wanaotaka kuchagia.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Mwegelo alisema mbali na michango ya fedha, Chama cha Wahandisi Wanawake kimejitolea kutoa ushauri wa namna ya kujenga mabweni hayo.

Mwegelo pia alisema katika kampeni hiyo, wako wadau waliochangia mabweni mawili yanayochukua wanafunzi 80 kila moja na lengo ni kujenga mabweni sita.

“Nawashukuru wananchi wa Tanzania na wadau wa maendeleo waliojitokeza kuchangia kampeni hii ya kuwakomboa watoto wa kike kwa kuwawekea mazingira wezeshi ya kupata elimu, ingawa kwa siku za usoni tutajenga na ya watoto wa kiume,” alisema.

“Kama mnavyojua, Machi ulikuwa mwezi wa wanawake na wilaya ya Kisarawe tukaona badala ya kuvaa sare na kusherehekea ni bora tuwe na kampeni itakayoinua wanawake wengi wa kesho ambao ni wanafunzi wa wilaya yetu wanaokabiliwa na changamoto mbalimbali zinazowafanya kushindwa kufikia malengo yao,” aliongeza.



Alisema pia kiwanda cha Sao Hill kimeahidi kutoa mbao za kuezeka mabweni hayo zenye gharama ya Sh. milioni 10 na kutoa mafunzo ya ufundi kwa kutengeneza samani kwa mgambo 40 wa wilaya hiyo.

Alitaja misaada mingine waliyopokea kuwa ni mifuko 1,890 ya saruji na tayari 1,050 imeshapokewa ofisini kwake na kontena moja la marumaru.

“Pamoja na kampeni hii iliyowezesha upatikanaji wa fedha pia kampeni hii imeenda sambamba na mafunzo ya walimu 220 ambao wafundishwa namna ya kutoa elimu inayoenda na karne ya 21 ya kuwawezesha wanafunzi wanaohitimu kujitegemea na kuwa viongozi wanaojitambua,” alisema mkuu huyo wa wilaya.

Pia alisema kupitia kampeni ya kuwaweka wanafunzi kambi kwa ajili ya kujisomea wanapokaribia kufanya mitihani ya kidato cha nne, imesaidia kuongeza ufaulu daraja la kwanza kutoka wanafunzi saba hadi 37 na waliopata sifuri kupungua kutoka wanafunzi 257 hadi wanafunzi 175.

Mwegelo pia alisema sababu ya kufanya kampeni hiyo ni kupunguza idadi ya wanafunzi wanaoshindwa kufika kidato cha sita. Katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2017, wanafunzi 4,880 walimaliza kidato cha nne lakini wanafunzi 66 ndio waliofika kidato cha sita.



Akinamama wachuuzi wa maparachichi wakiyapanga wakati wakisubiri wateja katika Mtaa wa Tandamti, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Ashinda kura za maoni CCM kurithi kiti cha Nassari

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wazazi (CCM) Mkoa wa Arusha, Dk. John Pallangyo, ameshinda kwa kishindo kinyang’anyiro cha kura za maoni ndani ya chama hicho kwa ajili ya kupata mgombea ubunge katika Jimbo la Arumeru Mashariki mkoani hapa.

Uchaguzi mdogo wa ubunge katika jimbo hilo lililokuwa likishikiliwa na Joshua Nassari wa Chadema, umepangwa kufanyika Mei 19 mwaka huu, baada ya Mahakama ya Kuu Kanda ya Dodoma kutupilia mbali

kesi iliyofunguliwa na Nassari la kupinga kung’olewa kwenye nafasi hiyo.

Spika wa Bunge, Job Ndugai alitangaza jimbo hilo kuwa wazi baada ya Nassari kushindwa kuhudhuria vikao vitatu vya Bunge mfululizo bila kutoa taarifa kinyume cha kanuni.

Katika uchaguzi huo uliofanyika jana katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, wagombea 33 wakiwamo wanawake watatu, walijitokeza kuchukua fomu kwa ajili ya kuwania kuteuliwa na chama hicho.

Akitangaza matokea hayo, msimamizi wa uchaguzi ambaye ni Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, ambaye pia ni mlezi wa chama hicho Mkoa wa Arusha, Humphrey Polepole,

alisema kati ya kura 690 zilizopigwa, Dk. Pallangyo aliibuka mshindi kwa kupata kura 470.

Polepole alisema mshindi wa pili ni Wakili Dk. Daniel Pallangyo, aliyepata kura 50 huku William Sarakikya akishika nafasi ya tatu kwa kupata kura 36.

INAENDELEA UK 8

# Upelelezi kesi ya Dk. Tenga waiva

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeambiwa kwamba upelelezi wa kesi inayowakabili vigogo wa Kampuni ya Six Telecoms, akiwamo Wakili Mwandamizi wa Kujitegemea, Dk. Ringo Tenga, na wenzake umekamilika.

Hatua hiyo ilifikiwa jana na upande wa Jamhuri mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Patrick Mwita, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kwamba Jamhuri inaandaa nyaraka kwa ajili ya mchakato wa kusikilizwa.

“Mheshimiwa Hakimu, kesi hii imepangwa kwa ajili ya kutajwa na Jamhuri tunaifahamisha mahakama kwamba upelelezi wake umekamilika, hivyo tunaandaa nyaraka kwa ajili ya kuanza mchakato wa kusikilizwa” alidai Mwita.

Kutokana na madai hayo, Hakimu Simba alisema kesi hiyo itatajwa Aprili 17, mwaka huu, na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mbali na Dk. Tenga, washtakiwa wengine ni Mhandisi na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Hafidhi Shamte maarufu Rashidi Shamte, mfanyabiashara na mkurugenzi wa kampuni hiyo, Peter Noni, Mkuu wa Fedha wa kampuni hiyo, Noel Chacha na kampuni ya Six Telecoms Limited ambao wanadaiwa kutakatisha Sh. bilioni nane.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashitaka sita yakiwamo ya utakatishaji wa fedha, hivyo kuwafanya wakae mahabusu kwa kuwa makosa hayo hayana dhamana kwa mujibu wa sheria.

MAHOJIANO MAALUM

# Mbatia ataja sababu Kamati ya Bunge kuonekana ya CCM

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

JUMANNE iliyopita, siku ya kwanza ya Bunge la Bajeti linaloendelea mjini Dodoma, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, alisema bungeni kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge inaonekana kuwa mali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mbowe alitoa kauli hiyo nzito alipokuwa anachangia hoja ya pendekezo la kamati huyo kuhusu Bunge kuazimia kutofanya kazi na Prof. Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambaye amekutwa na hatia ya kulidhalilisha, kulidharau na kulishushia heshima na hadhi Bunge kutokana na kauli yake ya mwanzoni mwa mwaka Newyork, Marekani kwamba anafikiri "huo ni udhaifu wa Bunge".

Katika mchango wake, Mbowe alisema uamuzi kuhusu Bunge kutofanya kazi na CAG Assad, ulikuwa umefanyika hata kabla ya kamati hiyo ya Bunge kupendekeza chombo hicho kitoke na azimio hilo.

Mwenyekiti huyo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) alisema inaonyesha wazi kwamba azimio hilo lilikuwa limeshafanyiwa uamuzi na kuamua kutumia vifungu vya katiba kutoa ushauri kwa Bunge hata kabla ya wabunge kuamua adhabu dhidi ya Prof. Assad.

"Kwa kuwa azimio hili limeshafanyiwa maamuzi, sitaongea mengi, nitaongea kwa kifupi sana, historia ambayo mnaiandika leo (Jumanne), Bunge mnalipa upungufu.

"Mnataka kuwaziba Watanzania midomo, watu wasiseme, wakati sisi hapa bungeni tunafanya maamuzi kwa niaba ya Watanzania, mnataka tudhulumu haki za msingi za watu kwa sababu tuna mamlaka ya kufanya hivyo," Mbowe alisema.

Alishauri Bunge kuangalia upya muundo wa kamati zake, akieleza kuwa kamati iliyomtia hatiani Prof. Assad, haiwezi kutenda haki dhidi ya vyama vya upinzani na watu wanaoonekana kwenda kinyume cha mtazamo wa serikali.

"Na katika siku za usoni, mnapounda kamati ya maadili, kama tuna nia njema na nchi yetu, muangalie 'composition' (muundo) ya kamati za maadili, kwa sababu 'composition' ya kamati ya maadili leo haiwezi ikafanya 'justice' kwa vyama vya upinzani au kwa watu wanaoonekana pengine wanaikwaza serikali," Mbowe alisema.

Mbowe alisema kuendelea kuweka wajumbe wengi kwenye kamati hiyo kutoka CCM, kutatoa mtazamo kwa umma kuwa Kamati ya Maadili ni kamati ya chama na uamuzi unafanyika nje ya Bunge kwa kuwa wajumbe wa kamati wanakuwa wanafuata maelekezo waliyopewa.

Katika mahojiano maalum na Nipashe mjini Dodoma juzi, Mwenyekiti wa Chama cha



NCCR-Mageuzi na Mbunge wa Vunjo, James Mbatia (pichani), aliunga mkono hoja hiyo ya Mbowe, akieleza kuwa tangu kuanza kwa Bunge la 11, hakuna hata mbunge mmoja wa CCM aliyefikishwa mbele ya kamati hiyo.

Mbatia alidai baadhi ya wabunge wa CCM wamekuwa wakifanya makosa yanayopaswa kushughulikiwa na Kamati ya Maadili, ikiwamo kuzomea, kutoa kauli za ovyo na kutukana bungeni, lakini hakuna hata mmoja aliyefikishwa mbele ya kamati hiyo katika miaka minne ya Bunge la 11.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na kiongozi huyo wa NCCR-Mageuzi:

**SWALI:** Mbowe amesema bungeni kuwa Kamati ya Maadili inaonekana kama mali ya CCM. Wewe ni mbunge mzoefu, nini maoni yako kuhusu kauli hiyo ya Mbowe?

**MBATIA:** Ninashukuru sana kwa swali na ili nilieleze vizuri, naomba kidogo nitengeze historia. Mimi ni mbunge ambaye pia ni mwanzilishi wa mageuzi ya nchi hii.

Nakumbuka Juni 11, 1991 tulikuwa na mkutano pale Diamond Jubilee (Dar es Salaam) tukidai kurejeshwa vyama vingi katika nchi yetu na namkumbuka kipindi kile, tulikuwa na mzee mmoja mwandishi mwenzenu wa habari, Ndimara Tigambwage. Aliandika vitabu viwili kwa sasa mngeandika 'paper' mbili; moja ilikuwa na kichwa cha habari 'Tutapingana Bila Kupigana' na kingine kilisema 'Upinzani Siyo Uadui'.

Sasa hili Bunge ni Bunge la upinzani, maana yake ni kwamba ni Bunge lenye mawazo kutoka chama tawala na vyama mbadala, sasa si mara zote mawazo ya vyama mbadala, nyie mnaita vya upinzani, yakakubalika kwa chama tawala.

Sasa, tafsiri ninazoziona hapa bungeni na ninaziona kwa awamu hii ya tano ni kwamba ukiwa na mawazo tofauti na watawala au ukiwa na mawazo tofauti na Bunge lenyewe, unaonekana kwamba wewe ni mkorofi, wewe huna heshima, wewe huna adabu, kwa hiyo, unashughulikiwa.

Lakini, Bunge la vyama vingi lenye wabunge kutoka vyama tofautitofauti na lazima mjue vyama vina sera tofauti, sasa ukapata wazo tofauti ukahisi kwamba ni tusi au ni ugomvi au ni namna gani.

Nichokiona katika hili Bunge ni kwamba wapinzani wanaonewa na kwa sababu wanaonewa ndiyo maana unaona zile 'reactions' (misuguano).

Nitawapa mfano, mjadala wa jana (Jumanne) kuhusu shauri la Kamati ya Maadili dhidi ya CAG, wabunge kutoka chama tawala walipewa nafasi ya miongozo wakati wabunge wa upinzani walivyokuwa wanajenga hoja zao, lakini ilipofika zamu ya wabunge wa CCM kuchangia, wabunge wa upinzani waliomba miongozo ilishindikana mpaka wakatumia utaratibu mwingine wa kuomba taarifa.

Sasa, taarifa na muongozo ni kitu tofauti, ukifanya namna hiyo, ina maana haki haitendeki na kama haki haitendeki, huwezi kuzuia hawa wengine 'ku-react'.

**SWALI:** Wewe ni kiongozi na ushawishi kwa wabunge wenzako wa upinzani kutokana na uzoefu wako bungeni. Mmechukua hatua gani kutatua changamoto hii?

**MBATIA:** Kuna mambo mengine sisi kama viongozi tunapaswa tuyashughulikie kama viongozi, mnaona kilichotokea asubuhi (Jumatano). Kwa maoni yangu kusingekuwa na sababu ya kumtoa Esther (Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini -Chadema) ndani eti kwa sababu tu kusema Spika hicho unachosema siyo sahihi.

Watu wengi wamezungumza pale, lakini pia kusingekuwa na sababu ya kutaja mkopo ambao (Godbless) Lema amechukua kwa sababu lazima mjue kukopa ni kuaminika, mtu ambaye huaminiki huwezi kukopeshwa na kukopa maana yake una uwezo wa kufanya kazi.

Na kwa kijana, mbunge kijana kama yule (Lema) kukopa anawaonyesha njia vijana wenzake kwamba tunaweza tukatoka katika umaskini kwa kutumia fedha ambazo zipo maeneo mbalimbali zikiwamo benki na mahali pengine. Lakini Spika aliitaja ile kwa sababu pengine alifikiri kwamba anamshughulikia. Sasa, hiyo siyo sawa ndiyo maana wabunge wa upinzani wameona siyo sawa.

Suala la Lema kupelekwa kwenye Kamati ya Maadili kwa kusema Bunge ni dhaifu halihusiani na mambo binafsi ya kwake, mambo ya mikopo yake, mambo ya maisha yake na vitu vingine kama hivyo.

Sasa, hili Bunge ni la Watanzania na linategemewa sana na Watanzania. Sasa, tukienda hivi, kitu cha kwanza tunaweka rekodi mbaya katika Bunge letu kwa sababu yote yanayojadiliwa haya, watoto wetu wengine watakuja kufanya, rejea kuangalia kuainisha na vitu kama hivyo.

Mimi naomba tu turejee kwenye hali yetu ya kawaida, sote ni Watanzania, sisi wote hapa tumekuja kujenga nchi yetu, tufanye kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na Spika kama kiongozi wa Bunge, anapaswa awaone wabunge wote kwamba ni wa kwake.

Ukipewa nafasi ya kuongoza, uwe Rais, uwe Spika, uwe baba wa familia, lazima ujue wale unaowaongoza kuna wenye akili, kuna wasio na akili, kuna wagonjwa, kula vilema na kila kitu, wote ni wa kwako.

Hii kamati mnayosikia ya maadili, upinzani nadhani wapo watatu tu. Mimi nimekaa kwenye Bunge hili kwa muda mrefu. Tangu Bunge hili limeanza, kwanza mimi ningekuwa mjumbe wa kamati, kwa heshima yangu ningetoka kwa sababu tangu kamati hii imeanza kwenye Bunge hili la 11, hakuna mbunge wa CCM hata mmoja ameshawahi kupelekwa kwenye hii kamati.

Kwa hiyo, ni kama kamati imeundwa kwa ajili ya kuwashughulikia wabunge wa upinzani, lakini kinachotokea bungeni, wabunge wa upande mwingine wanawatukana sana wabunge wa upinzani, wanapiga kelele sana, lakini hakuna hata mmoja wao aliyefikishwa mbele ya kamati hii.




**HABARI KITAIFA**

# Wawekezaji walilia gesi Mtwara

**Na Romana Mallya**

ZAIDI ya kampuni kubwa 30 za uwekezaji katika sekta ya mafuta zimeiomba serikali kuharakisha mradi wa kuchakata gesi asilia mkoani Mtwara.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam wakati Bodi ya Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) ilipokutana na wafanyabiashara hao ikiwa ni mwendelezo wa kukaa na taasisi mbalimbali kujadiliana na kubaini changamoto za wafanyabiashara ambazo huwasilishwa serikalini ili zitatuliwe.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, akizungumza kwenye mkutano huo, alisema moja ya changamoto ambazo zimeonekana ni ya mradi wa kuchakata gesi asilia, kutokuwa na dalili za kuendelea.

"Tumekutana na sekta ya mafuta na gesi ili kujadili changamoto zao na moja ya changamoto waliyotueleza ni mradi wa kuchakata gesi Mtwara, hivyo tunaomba serikali iuharakishe," alisema. Pia alitaja changamoto nyingine iliyoainishwa kwenye mkutano huo kuwa ni mikataba ya makubaliano ya uzalishaji na mauzo ya gesi na mafuta (PSA) ambayo serikali iliichukua ili kuiangalia upya ambayo alisema imechukua muda mrefu.

"Wametueleza kuwa mikataba hii ilichukuliwa na serikali na wao wanalalamika kuwa suala hilo limechukua muda mrefu, hivyo wanaomba kuharakishwa," alisema.

Simbeye alisema wiki tatu zilizopita TPSF ilikutana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye aliahidi mpaka mwishoni mwa mwezi huu, kazi ya kuipitia mikataba hiyo itakuwa imekamilika.

Alisema michakato ya aina hiyo serikalini ni ya kawaida na imeshafanyika pia kwenye sekta ya madini kuipitia mikataba ya nyuma iliyokuwa imeingiwa baina ya serikali na wawekezaji.

Mjumbe wa Bodi ya TPSF, Balozi Abdulsamad Abdulrahim, ambaye pia ni Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Watoa Huduma wa Sekta ya Gesi na Mafuta Tanzania, alitaja changamoto zingine zinazokabili sekta hiyo kuwa ni usumbufu wanaopata kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), baadhi ya viongozi kuwasumbua wawekezaji ambalo Rais John Magufuli alishalizungumzia suala hilo.

Alitaja changamoto nyingine ambayo wawekezaji sekta hiyo wameieleza ni mikataba ya kazi, malimbikizo ya madai yao ya kodi.




Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya GSM, Fatma Abdallah (katikati), akikata keki kuzindua bidhaa mpya ya hamira, katika hafla iliyofanyika, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mwakilishi wa kampuni ya Anchor ya Afrika Kusini, Oscar Mohlabe na Mkuu wa Mauzo na Masoko wa kampuni hiyo, Allan Chonjo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wataka udhibiti mwendokasi hifadhini

**Na Novatus Makunga,** SERENGETI

WATAALAMU wa mradi wa utafiti wa duma nchini wametaka mwendokasi wa magari yanayobeba watalii udhibitiwe ndani ya hifadhi za taifa kwa madai ya kusababisha kugongwa mara kwa mara wanyamapori hasa adimu waliopo hatarini kutoweka.

Ushauri huo ulitolewa juzi na timu ya wanasayansi waliopo katika mradi unaoratibiwa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (Tawiri), ambao kwa sasa wanaendelea na utafiti wa kupungua kwa duma katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Mratibu wa mradi huo, Denis Minja, alisema kati ya mwaka 2016 na 2018 duma wapatao wanane walikufa kutokana na kugongwa na magari ya watalii Serengeti.

"Duma wanne waligongwa na kufa Serengeti mwaka jana na katika mwaka 2017 watatu waligongwa huku mwaka 2016 aligongwa mmoja na kufa," alisema.

Minja alisema pamoja na adhabu ya faini ya dola za Marekani 5000 (zaidi ya Sh. milioni 11) na kuzuiwa kuingia katika hifadhi ya taifa kwa miezi mitatu kwa dereva wa gari, alisisitiza bado ajali hizi ni janga kubwa kwa utalii. "Jaribu kupiga hesabu nyepesi tu, kasi ya duma ni kilometa 105 kwa saa na ana uwezo wa kuchanganya kasi hiyo kwa muda mfupi tu, hivyo kugongwa kwao mara kwa mara kunaashiria kuna tatizo," alisema Minja.

Alishauri ni vyema sasa ukawapo mfumo au vifaa vya kudhibiti mwendokasi wa magari hususani katika hifadhi ya taifa ya Serengeti. Minja alisema duma ni kati ya wanyama 10 adimu aina za paka mwenye kasi sana duniani na pia ni hatari na kwamba asilimia tisa tu ya aina hiyo ya mnyama ndio wamebakia katika historia ya wanyama hao duniani.

Aidha wataalamu hao wa watafiti walitaja sababu nyingine za kupungua kwa duma ni kwa watoto wake kuliwa na wanyama wakali ambao wamewataja kuwa ni pamoja na fisi, simba na chui.

"Kimsingi kati ya watoto 100 wa duma wanaozaliwa ni asilimia tato tu ndiyo wanaoweza kuendelea kuishi," Minja alifafanua.

Watafiti wanasayansi hao wanataja sababu nyingine ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi, ujangili, ongezeko la shughuli za kibinadamu na kasi ya ujenzi wa mahoteli ndani ya hifadhi za taifa.

"Kwa hali hiyo ni dhahiri kwamba kuna hatari kwa duma kutoweka duniani iwapo hatua za kumlinda hazitachukuliwa na katika nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania," Minja aliongeza.

Allibainisha katika mfumo wa Ikolojia ya Selous-Mikumi, duma wametoweka kabisa tangu miaka ya 1980. Minja alisema kuwa Tawiri inatarajia kuanza utafiti mwingine wa duma katika mfumo wa Ikolojia ya Ruaha-Rungwa pamoja na ikolojia ya Tarangire-Manyara. Katika nchi za Afrika ya Mashariki takwimu zinaonyesha kuwepo kwa duma 2,572 wanapatikana katika hifadhi za Serengeti na Ngorongoro pamoja na mbuga ya Maasai Mara na Tsavo nchini Kenya.

# Uganda yaipa tano Tanzania usimamizi rasilimali madini

**Na Rose Jacob,** MWANZA, GEITA.

UJUMBE wa Rais Yoweri Mseveni wa Uganda ukiongozwa na Waziri wa Nishati na Maendeleo ya Madini, Peter Crolies, umekiri kuwa uwekezaji wa Tanzania katika sekta ya madini ni mfano wa kuigwa na nchi zingine za Afrika.

Clories alisema hayo juzi katika ziara ya mafunzo ya siku nne katika mikoa ya Mwanza na Geita, iliyokuwa na lengo la kujifunza Tanzania inavyoendesha sekta ya madini na kufanikiwa kuwa na uhusiano mzuri baina ya serikali na wachimbaji wadogo na wakubwa kwa kudumisha amani.

"Tanzania na Uganda zitaendelea kushirikiana katika nyanja za teknolojia na taarifa za kijiolojia. Tumekuja hapa kujifunza juu ya usimamizi wa rasilimali za madini ili nasi kupata ujuzi kutoka Tanzania ambao tutaenda kuifikishia kwa serikali yetu na kuwafundisha wananchi wetu wanaojihusisha na uchimbaji wa madini," alisema Crolies.

Crolies alishukuru na kuufurahia urafiki wa Tanzania na Uganda kati ya Rais Museveni na Rais John Magufuli ambao alisema umeonyesha manufaa makubwa yenye tija kwa wananchi wa nchi hizo mbili.

Alisema ziara hiyo imekuwa ya mafanikio kwao kwa kuwa hawajawahi kushuhudia na kujifunza rasilimali za madini zinavyotakiwa kuendeshwa na kutunzwa hadi kufikia hatua ya jamii na serikali kupata uchumi mzuri.

Naye Naibu Waziri wa Madini, Stansalaus Nyongo, alisema wachimbaji wadogo ndio watoroshaji wakubwa wa madini hususan dhahabu, lakini Tanzania imejipanga kudhibiti na kuangalia namna ya kupunguza utoroshaji huo.

"Waganda wameona vizuri kuja Tanzania kujifunza kuhusu madini kutokana na sisi kutunza vizuri rasilimali za madini hasa kwa wachimbaji wadogo ambao imekuwa vigumu kwa nchi zingine kufanya kazi kwa ushirikiano na kudumisha amani," alisema Nyongo. Ujumbe huo uliokuwa na maofisa waandamizi kutoka serikali ya Uganda pamoja na wachimbaji wadogo 35, ulitembelea maeneo yanayochimbwa dhahabu katika migodi ya GGM, Rwamgasa,

Busorwa Mine, Nsagano na maeneo ya kuchenjulia dhahabu ya Rich Hill na Genge Tatu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba fanyeni haya leo Mazembe ing'oke Caf

**LEO** wawakilishi pekee wa Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, watashuka Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kuikaribisha TP Mazembe katika mechi ya robo fainali ya michuano hiyo.

Simba imetinga hatua hiyo baada ya kushika nafasi ya pili ikiwa pointi moja nyuma ya vinara Al Ahly ya Misri kutoka Kundi D lililokuwa likijumuisha pia AS Vita ya DR Congo pamoja na JS Saoura ya Algeria. Wawakilishi hao pekee wa Afrika Mashariki na Kati wataivaa TP Mazembe wakiwa na rekodi nzuri ya kushinda kwa asilimia 100 katika mechi zake zote za nyumbani kwenye michuano hiyo msimu huu. Hiyo ni kutokana na kuichapa JS Saoura kwa mabao 3-0 kisha ikaikalisha Al Ahly kwa bao 1-0 kabla ya kukamilisha hatua ya makundi kwa kuwakalisha ndugu wa nchini moja na TP Mazembe, AS Vita kwa mabao 2-1.

Hata hivyo, pamoja na rekodi hiyo ya kuvutia katika Uwanja wa Taifa, Simba imeongoza kwa rekodi mbovu zaidi kwenye kundi lao si tu kwa kupoteza mechi zote za ugenini kama ilivyo kwa AS Vita, bali pia kwa kuruhusu mabao mengi zaidi.

Katika mechi za ugenini, Simba imeruhusu mabao 12, ikikubali Kulala 5-0 dhidi ya AS Vita na idadi kama hiyo kutoka kwa Al Ahly ilipoifuata Misri kabla ya kuchapwa 2-0 nchini Algeria na JS Saoura. Rekodi hiyo ya Simba nyumbani inatupa matumaini makubwa ya kuishuhudia tena ikiiendeleza leo kwa kuichapa TP Mazembe Uwanja wa Taifa.

Lakini pamoja na matumaini yetu makubwa kwa Simba leo, pia tunaitaka kuongeza kasi katika safu yake ya ushambuliaji kwa kutumia vema kila nafasi wanayoipata ili kujipatia mabao mengi kadri iwezekanavyo. Tunayasema hayo kutokana na ukweli kwamba hatua hii sasa ni ya mtoano na kitakachoweza kuisaidia Simba na kuweza kusonga mbele ni idadi kubwa tu ya mabao na si pointi tena.

Hivyo, kutokana na rekodi mbovu ya Simba kutoweza kupata bao ugenini hadi sasa katika hatua ya makundi ya michuano hiyo, njia pekee ya kuweza kuitoa TP Mazembe na kutinga nusu fainali ni kushinda kwa idadi kubwa ya mabao ikiwa nyumbani.

Lakini pia safu yake ya ulinzi ikijitahidi na kuhakikisha hairuhusu bao nyumbani kabla ya Aprili 12, mwaka huu kwenda DR Congo kurudiana na TP Mazembe.

Nipashe tunaamini kama Simba itaweza kupata ushindi wa kishindo na kutokubali kuruhusu bao Taifa, mechi ya marudiano itakuwa rahisi kwao kuweza kuulinda na hatimaye kusonga mbele. Aidha, wakati wachezaji wakijitahidi kulitekeleza hilo, wadau wa soka, wanachama na mashabiki wa Simba pamoja na Watanzania kwa ujumla hawana budi kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu hiyo. Kama ambavyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli alivyosema wakati akiipongeza Taifa Stars kwa kufuzu Afcon 2019, kuwa mashabiki wa Yanga na Simba wanapaswa kuungana na kuwa kitu kimoja wakati timu mojawapo inaposhiriki michuano ya kimataifa, ndiyo ambavyo Nipashe tungependa kuliona hilo likianza kutekelezeka leo.


Ikimbukwe Simba inaposhiriki michuano hii ama ikitokea Yanga kushiriki, hupeperusha bendera ya Tanzania, hivyo ni sifa kwa Taifa letu kutoa klabu inayofanya vizuri, lakini pia mafanikio ya 'Wekundu wa Msimbazi' hao ni ya Yanga pia kwani ikisonga mbele itaifanya Tanzania kuongezewa timu moja kwenye michuano hii msimu ujao. Kadhalika, pamoja na matumaini yetu kwamba mashabiki watajitokeza kwa wingi, lakini kujitokeza kwao tungependa kuona kukienda sambamba na ushangiliaji mwanzo mwisho kwa dakika zote 90 za mchezo.

Hatutaraji kuona tena mashabiki wakisubiri hadi lifungwe bao ama timu kupiga pasi za kuvutia ndipo mashabiki waanze kushangilia na Simba inapotanguliwa kufungwa wakikaa kimya kama vile wamemwagiwa maji, bali tunataka kuona ushangiliaji usiokoma Taifa leo. Kila Kheri Simba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba, Yanga wajua tamu ya ua, sumu wanipiani?

Na Barnabas Maro

**UNAJUA** kuwa ua ndilo lenye utamu, kwa nini ukanipa sumu? Huweza kutumiwa kwa mtu anayemfanyia mwenzake jambo baya ingawa analifahamu lililo zuri.

Hii ni maalumu kwa wanachama na mashabiki wa Simba na Yanga wanaohujumiana, kufurahia na kuchekana wakati mojawapo inaposhindwa na timu ngeni kutoka ughaibuni (nchi zilizoko mbali).

Simba na Yanga wamekuwa kama "udugu wa nazi kukutana chunguni." Ni methali ya kutumiwa kuwapigia mfano watu wasioweza au wasiopenda kushirikiana hadi inapokuwa wakati m-baya sana, tena wanapokuwa wamechelewa! Yafaa kutambua faida ya kushirikiana mapema. Bila kumunyamunya (chezesha midomo kama mtu anayetaka kuongea au kucheka), moja ya timu hizo inapopambana na timu kutoka ughaibuni, hupata mashabiki wa timu pinzani humu nchini kwa kuishangilia na kuizomea timu ya nyumbani. Timu za nchi na jiji moja lakini zachukiana kupita kiasi.Yashangaza, lakini ndio ukweli wenyewe!

Hebu tuache ujinga huu kwani ni sawa na kujicheka mwenyewe kwani Simba na Yanga zote ni za Tanzania ilhali timu ngeni huja na kurejea makwao na kutuacha na uzuzu (uwezo mdogo wa mtu kufahamu mambo; hali ya mtu kutojua jambo linaloendelea) wetu kwani wajinga ndiwo waliwao. Wenzetu huko nje hawana uzuzu (hali ya kutoweza kufahamu hata baada ya kuelezwa vizuri) huo.

Mwaka huu Tanzania inawakilishwa na timu tatu kwenye michuano ya kimataifa: Taifa Stars, Serengeti Boys na Simba SC. Ni faraja iliyoje kwa Watanzania kuwakilishwa na timu tatu? Ni wakati wa kushirikiana kwa hali na mali ili kuitambulisha Tanzania kuwa kwa kandanda Afrika nasi tumo.

Twapaswa kuwa wamoja kwa kuzishangilia na kuzitia hamasa timu zetu kwani zikishinda sifa itakuwa kwa Tanzania yote wakiwamo hao waitwao 'watani wa jadi' kumbe ni 'maadui wa jadi!' Tumechoka kuwa 'vichwa vya wendawazimu' huku timu ngeni zikizigeuza timu zetu kama jamvi la wageni litumiwalo na wageni wanaokuja nchini! Tutazinduka lini na ubozi huu?

Hii yanikumbusha methali ya "Siteti na mwandaniwa kwa mtu mweni (mgeni) wa leo." Mwandaniwa ni mwendani wangu. Maana yake sigombani na rafiki yangu au mwandani wangu kwa sababu ya mgeni ambaye yupo kwa muda mfupi tu. Methali hii huweza kutumiwa kutukumbusha umuhimu wa kutowaudhi marafiki zetu tunaowategemea kila siku kwa kuwa tumempata rafiki wa muda tu.

Leo Simba itapambana na timu ya TP Mazembe kutoka Congo (DRC) jijini Dar es Salaam na mechi ya marudiano itafanyika ugenini DRC. Ni muhimu Simba watambue kuwa "Awali ni awali, hakuna awali mbovu." Kwamba mwanzo ni mwanzo hapana mwanzo unaosemekana kuwa m-baya. Binadamu aanzapo jambo keshalianza; iwe vibaya au vizuri. Methali hii yawashauri Simba wawe na tabia ya kuanza kufanya jambo au kuwahi mambo wanapokuwa nyumbani. Nawajibika kuwakumbusha Simba kuwa "Mcheza hawi kiwete, ngoma yataka matao." 'Matao' ni mbwembwe na machachari. Maana yake mtu anayecheza ngoma hawi na kilema kwa kuwa uchezaji ngoma una machachari mengi.

Nawanasihi wachezaji wa Simba kwamba waazimiapo ushindi lazima wacheze kwa juhudi kubwa bila kukata tamaa. Hawapaswi kuwa walegevu au kufanya ajizi kwani ajizi ni ufunguo wa umasikini. Pia wakumbuke kwamba "mcheza kwao hutuzwa." Mtu anayecheza kwao hupewa zawadi au hutunzwa vizuri.

Ili kujenga jina la Tanzania, ni muhimu Watanzania wote kuweka kando itikadi (imani) zao na kuwa wamoja katika kuzishangilia timu zetu zinazoliwakilisha taifa ikiwamo klabu ya Simba waitwao 'Wekundu wa Msimbazi'. Nina uhakika kuwa endapo Simba watatwaa ubingwa wa Afrika, itakuwa changamoto kubwa kwa wenzao wa Yanga na wengine ili nao wajibidishe kufanya vivyo hivyo.

Hayo ndio maendeleo badala ya kukaliana 'mguu-kausha,' kuchukiana na kuombeana mabaya. Unapomwombea mwenzio mabaya unafaidika nini? Ni yale yasemwayo 'bora tukose wote!' Ikiwa hivyo unanufaika kwa lipi? Hata wahenga walisema "Adui mpende." Maana yake usimchukie adui wako. Ni vizuri kuwasamehe maadui zetu yamkini huweza wakauona ubaya wao na kubadilika.

"Usifurahi adui yako aangukapo, wala moyo wako usishangilie ajikwaapo; Bwana asije akaliona hilo likamkasirisha, akageuzia mbali naye hasira yake." (Mithali 24: 17-18). "Adui yako akiwa na njaa, mpe chakula, tena akiwa ana kiu, mpe maji ya kunywa; maana utatia makaa ya moto kichwani pake, na Bwana atakupa thawabu." (Mithali 25: 21-22).

Wahenga walisema: "Jamala mno ni utu sifa ya ndege si mbawa." Jamala ni wema au uzuri. Hujajua maana yangu? Aliye juu mngoje chini. Vijana wa mjini husema 'kutesa kwa zamu.'

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akizungumza na Naibu Spika wa Bunge la Cameroon na Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kimataifa (CPA), Emilia Monjowa Lifaka, alipomtembelea ofisini kwake, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Regista watu wenye ulemavu kuanzishwa

SERIKALI imesema inakamilisha uanzishwaji wa regista ambayo itasaidia kupata takwimu sahihi za watu wenye ulemavu katika maeneo yote ya mijini na vijijini.

Kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), idadi ya walemavu nchini ni zaidi ya milioni 2.6.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Watu wenye Ulemavu, Stella Ikupa, alisema hayo jana bungeni mjini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kinondoni (CCM), Maulid Mtulia.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema walemavu wana mahitaji maalum kulinganisha na watu wasiokuwa na ulemavu na idadi ya walemavu imekuwa ikiongezeka siku hadi siku kutokana na ajali za barabarani hasa zitokanazo na usafiri wa bodaboda. "Je, serikali inaweza kuorodhesha idadi ya walemavu nchini kwa kuzingatia makundi yao kwa asilimia? Je, serikali ina mpango gani mahsusi wa kuwajengea uwezo wa kujitegemea walemavu wote hasa vijana, watoto na wanawake ili kuondoa utamaduni wa walemavu kuendesha maisha yao kwa kuombaomba?"alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema faida nyingine ya kuanzishwa rejista hizo ni kutambua sababu za kuongezeka kwa ulemavu katika kila eneo na changamoto zinazowakabili.

Alisema katika kuhakikisha watu wote wenye ulemavu hasa vijana, watoto na wanawake hawaachwi nyuma kiuchumi, serikali inaendelea kuwajengea uwezo kuhakikisha watoto wote ikiwa ni pamoja na wenye ulemavu wanapata elimu ya msingi na sekondari ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea.

"Pia inatoa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa makundi ya vijana na wanawake wenye ulemavu kupitia vyuo vya watu wenye ulemavu na program ya kukuza ujuzi hapa nchini,"alisema.

Alibainisha kuwa kati ya idadi hiyo, watu wenye ualbino ni 16,477 sawa na asilimia 0.04.

Alifafanua kuwa wenye ulemavu wa kuona ni 848,530 (asilimia 1.93, usikivu 425,322 (asilimia 0.97), kutembea 525,019 (asilimia 1.19), kukumbuka 401,931 (asilimia 0.91), kujihudumia 324,725 (asilimia 0.74), na ulemavu mwingine 99,798 sawa na asilimia 0.23.

Aidha alisema ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanawezeshwa kiuchumi, serikali inatoa mkopo wa fedha ya asilimia mbili zinazotokana na mapato ya ndani ya halmashauri.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuwajengea uwezo ili kupunguza matumizi ya viungo bandia.

Akijibu swali hilo, Ikupa alisema kuwa serikali imekuwa na mipango mingi kwa watu wenye ulemavu ikiwamo kuwapa vifaa visaidizi na kwa kuliangalia hilo imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili hiyo. Akiongezea majibu, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile amesema Serikali imeondoa kodi kwa watu wenye ulemavu.

Aidha alisema kuanzia mwezi huu kitengo cha mifupa moi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), kitaanza upimaji na utoaji viungo bandia kwa walemavu wanaohitaji.




**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

# Viwanda viwili vya mhogo kukamilika Juni

BUNGE limeelezwa kuwa kabla ya kufikia Juni, mwaka huu, viwanda viwili vipya vya kusindika mhogo vitafunguliwa katika mikoa ya Lindi na Pwani.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tanga Mjini (CUF), Mussa Mbarouk.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema wakazi wa kata za Kirare, Tongoni, Mzizima, Chongoleani, Mabokwenu na Pongwe wilayani Tanga ni wazalishaji wakubwa wa mhogo lakini hawana soko la uhakika.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kutafuta soko la uhakika la mhogo ndani na nje ya nchi. Zipo mashine za kuchakata mhogo lakini bei zake ni kubwa na hivyo wakulima hawana uwezo wa kununua. Je, serikali haioni haja ya kuondoa kodi katika mashine hizo?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Kakunda alisema kutokana na ukweli huo kasi ya ujenzi wa viwanda vya kusindika muhogo ni kubwa.

Alibainisha mwaka huu peke yake mbali na viwanda vitano vinavyonunua mhogo kutoka kwa wakulima kwa sasa kuna viwili vipya vitakuwa vimefunguliwa kabla ya Juni, mwaka huu.

Alifafanua kuwa serikali imeweka vipaumbele vitatu ambavyo ndivyo vinavyowekewa msisitizo wa uwekezaji kwenye sekta ya viwanda.

Alitaja vipaumbele hivyo kuwa ni viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ili kuongeza thamani sambamba na kulinda jasho la mkulima.

"Cha pili ni viwanda vya kutengeneza bidhaa za nyumbani kama vyakula, nguo, samani na bidhaa tegemezi kwenye sekta ya ujenzi kama saruji, mabati ili kuharakisha ubora wa maisha na maendeleo na cha tatu ni viwanda vinavyoajiri watu wengi kwa ajili ya kuhakikisha ajira kwa vijana,"alisema.

Kadhalika, alisema zao la muhogo ambalo ni maarufu kwenye mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara na maeneo mengi ya nchi hadi Kigoma kwa sasa limepewa kipaumbele maalum duniani.

Alisema kutokana na ukweli kwamba muhogo hausindikwi kutengeneza unga wa ugali au uji au mkate au biskuti peke yake bali unatumika kwa sasa kwenye uunganishaji wa chuma, mbao, kutengeneza gundi na matumizi mengine mengi.

Aliongeza kuwa soko la muhogo Ulaya, Marekani na China ni kubwa sana kwa sasa na kwamba China pekee onahitaji tani milioni 2.5 za zao hilo kwa mwaka.

## Serikali kuandaa kitabu cha madini

WIZARA ya Madini kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST), inakamilisha uandaaji wa kitabu cha madini yanayopatikana Tanzania ili wachimbaji watambue maeneo ya madini.

Hayo yalibainishwa jana na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Stanslaus Nyongo, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Buyungu (CCM), Christopher Chiza.

Katika swali lake, Chiza alisema katika wilaya ya Kakonko kuna wachimbaji wadogo wa dhahabu katika vijiji vya Nyamwilonge, Nyakayenzi, Tuhuru na kuna dalili za kuwepo madini hayo katika sehemu zingine. Aidha, alisema kuna madini ya chokaa katika milima ya Nkongongwa ambayo yana matumizi mengine ya viwandani.

"Je, serikali imejipangaje kufanya utafiti wa uwepo wa madini na kuwasaidia wachimbaji wayachimbe na kujipatia kipato?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Nyongo alisema kitabu hicho ambacho ni toleo namba nne kitaonyesha uwapo wa madini katika mikoa, wilaya na vijiji na hivyo kusaidia wananchi na wachimbaji wadogo katika kutambua madini yaliyopo katika maeneo yao na matumizi yake.

Aidha alisema serikali itaendelea kufanya tafiti zaidi za jiosayansi katika mwaka 2019/20 kwenye maeneo ya Ruhuru na Nkongongwa katika wilaya ya Kakonko ili kubaini madini yaliyopo katika maeneo hayo.

Nyongo alisema pia wizara itatoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu njia bora za uchimbaji na uchenjuaji ili waweze kuelewa kuhusu jiolijia na madini yaliyopo kwenye maeneo yao. "Nyingine ni kuwashauri namna bora ya kufanya uchimbaji na uchenjuaji salama, wenye tija kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidika na rasilimali madini zilizopo katika maeneo yao,"alisema.

Alibainisha serikali kupitia taasisi hiyo ilifanya tafiti za upimaji uliofanyika mwaka 1960 na kuchora ramani ya jiolojia ya QDS 43(Kakonko).

Alisema mwaka 1978 hadi 1980 serikali ilifanya utafiti wa jiofizikia kwa kutumia ndege na kufanya uchakataji wa takwimu zilizochukuliwa na hatimaye kuainisha maeneo yenye mipasuko na miamba inayoashiria uwepo wa madini mbalimbali katika maeneo ya Kakonko na taarifa hizo zipo katika ofisi ya GST.

Alieleza kuwa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ikiwemo mradi wa Nordic fund, kampuni ya Beak Consultants GmbH ya Ujerumani na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kati ya mwaka 2003 na 2014 walifanya utafiti wa jiosayansi na kubainisha mambo mbalimbali.

Alitaja mambo hayo kuwa ni pamoja na uwepo wa madini ya dhahabu katika kata za Muhange kijiji cha Mwiruzi, Nyamtukuza, Nyamwilonge, Msekwa/Galama, Kasela na Kata ya Kasunga katika kijiji cha Nyakayanzi.

Aidha, alisema madini ya Agate katika kata ya Kasanda kijiji cha Nkuba kata ya Gawanumpu katika kijiji cha Kabingo na kata ya Nyamtukuza vijiji vya Nyamwilonge na Kasela.

HABARI KITAIFA

# Ashinda kura za maoni CCM kurithi kiti cha Nassari

INATOKA UK 3

Alisema wagombea wengine walipata kura kuanzia 26 hadi sifuri si kwamba hawana sifa za kuwa wagombea ubunge na kwamba kura alizopata mshindi wa kwanza si kigezo cha kumfanya awe mgombea wa CCM kwa sababu bado kuna vikao vya kujadili wagombea hao na majina yote yatajadiliwa.

"Wagombea wote bado mna sifa za kuwa wagombea ubunge kwa sababu vikao bado vipo vingi vya kujadili majina haya kwa kina ikiwa ni pamoja na kuchunguza kama mgombea aliyepata kura nyingi amezipata kwa njia halali," alisema.

Naye Katibu wa CCM Wilaya ya Arumeru, Shaaban Mdoe, alisema wagombea wote walikubaliana na matokeo hayo ambapo kila mmoja alisaini na kuridhika kuwa uchaguzi huo ulikuwa huru na haki.

Aidha, aliwataka wagombea hao wakati wakiendelea kusubiri vikao vya maamuzi kutofanya kampeni za aina yeyote ile wala kuchafuana kwa njia yeyote kwa sababu bado mchakato ni mrefu wa kuwajadili kwenye vikao ndani ya CCM.

Mdoe alitoa rai kwa wana CCM wilayani humo kukubaliana na mgombea atakayeletwa kupeperusha bendera ya CCM baada ya vikao vya uteuzi kumaliza kazi yake.

"CCM haina mtoto wa mgongoni wala wa tumboni wagombea wote ni sawa hivyo niwaombe wana CCM wenzangu kuepuka kuwa na makundi wakati wa kampeni na badala yake washirikiane na uongozi kuhakikisha CCM inapata ushindi wa kishindo," alisema.

Akizungumza baada ya kuibuka mshindi katika uchaguzi huo, Dk. Pallangyo aliwashukuru wana CCM wote waliomwamini na kumpa kura nyingi zilizompa ushindi wa kishindo na kwamba uchaguzi huo ulikuwa wa huru na haki.

"Nawashukuru wana CCM wenzangu kwa kuniamini na kunipa ushindi wa kishindo uchaguzi ulikuwa wa haki kura zimehesabiwa bila changamoto yeyote na wagombea wezangu wameridhika na kukubali kusaini matokeo ya uchaguzi huu," alisema.

Katika uchaguzi huo, ulinzi uliimarishwa nje na ndani ya ukumbi lengo likiwa ni kuhakikisha hakuna makada wanaoingia kwenye eneo hilo ambao walikuwa siyo wajumbe wa mkutano huo mkuu.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Paramagamba Kabudi (kulia) na Balozi wa China hapa nchini, Wang Ke, wakiweka mashada ya maua katika mnara wa makaburi ya Wachina waliofariki wakati wakijenga Reli ya TAZARA, katika hafla ya miaka 45 ya kumbukumbu, iliyofanyika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MAELEZO**

# Serikali yabanwa ukosefu ajira

INATOKA UK 2

katika taasisi hiyo, akieleza kuwa yeyote aliyeugua ama kuuguliwa na kufika kwenye taasisi hiyo, atakubaliana naye kwamba huduma zake ni bora.

Kutokana na ushuhuda huo wa Sakaya bungeni, Spika Ndugai alisimama na kusema Bunge litaandika barua kuipongeza JKCI kwa huduma nzuri.

Mbunge wa Viti Maalum, Anatropia Theonest (Chadema), alisema Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imekiuka sheria kwa kutoboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu uliopita.

Theonest pia alisema NEC imekuwa haitendi haki kwa watu wanaoomba kuchaguliwa kuwania nafasi za ubunge na udiwani wakati wa uchaguzi mdogo kutokana na maofisa wake kufunga ofisi na kujificha ili wagombea wa upinzani wasipate nafasi ya kurejesha fomu.

Mbunge wa Viti Maalum, Sonia Magogo (CUF), alisema kuna haja mashirika ya umma yakasimamiwa vizuri ili yatoe gawio kubwa ka serikali.

"Serikali inawekeza katika mashirika ya umma. Mwaka jana baadhi ya mashirika haya yalitoa gawio zuri kwa serikali. Kuna haja Msajili wa Hazina kuyasimamia vyema mashirika haya ili yatoe gawio maradufu mwaka huu," alisema.

Mbunge wa Kuteuliwa, Abdallah Bulembo (CCM), aliitaka Wizara ya Madini kutowafumbia macho wanaohujumu dhamira ya wachimbaji wadogo kulipa kodi na kutorosha madini.

Mbunge wa Muheza, Adadi Rajab, alisema ipo haja Mamlaka ya Mapato (TRA) kuangalia namna inavyotoza viwango vya kodi kwa kuwa wafanyabiashara wengi wa nguo wamekimbilia Uganda.

Alisema hata mwekezaji wa Kiwanda cha Pembe kinachozalisha ngano, amekifunga kutokana na kudaiwa kodi kubwa na TRA.

# Magufuli amshtukia mkandarasi

INATOKA UK 2

Pia alifananisha thamani ya ujenzi wa majengo hayo na ujenzi wa majengo ya chuo kingine cha ufundi stadi kilichojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 4.2 fedha ambazo zilitumika kujenga madarasa matano, nyumba 11 za walimu, ukumbi wa mikutano, bwalo la chakula na maabara.

"Kuna mambo yamejitokeza hapa huenda huyu mkandarasi amejichanganya au fedha zimepigwa. Naomba umalizie kazi iliyobaki na zingine ambazo sijaona wakati wa kukagua na fedha zitakazobaki utajenga na mabweni," alisema Rais Magufuli.

Akizungumzia makandarasi wazawa kutokuwa waaminifu, Rais Magufuli alitoa mfano kuwa kati ya makandarasi 8,000 waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa makandarasi (CRB), kwa mujibu wa sheria nchini ni asilimia 40 tu wanatumiwa kwenye kazi za ndani na asilimia 60 wanatoka nje ya nchi.

Akijitetea, mkandarasi huyo alidai bado hajakamilisha kazi na hadi sasa serikali imeshamlipa Sh. bilioni nne na zilizobaki ni zaidi ya Sh. bilioni moja na kwamba atazitumia kukamilisha ujenzi katika maeneo ambayo hawajakamilisha.

Awali, Rais Magufuli alizindua barabara ya Namtumbo, Kilimasela, Matemanga hadi Tunduru mkoani Ruvuma yenye urefu wa Kilometa 193 iliyojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 173.3.

# Bunge labariki

INATOKA UK 2

na usalama wa nchi kupitia mienendo ya vyama vya siasa.

Giga pia alizungumzia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), akieleza kuwa kamati yake inaendelea kuishauri kuboresha daftari la wapiga kura na kuchukua jitihada za kutosha kwa uangalifu katika kuliboresha.

"Hatua hizo zijumuishe utoaji elimu ya uraia hususan uandikishwaji wapigakura vijana wengi zaidi ili waweze kutumia haki yao ya kikatiba kupiga au kupigiwa kura," alisema.

Kiongozi huyo wa kamati pia alisema NEC inapaswa kufanya kazi kwa weledi ili kuendelea kuaminika kwa wadau wake wa uchaguzi.

"Tume ihakikishe inafuatilia wasimamizi wake wa uchaguzi na kuwawajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa.

"Kamati inaishauri serikali kuhakikisha inatoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati kuwezesha NEC kuratibu masuala mbalimbali ya uchaguzi kwa ufanisi," Giga alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, Oscar Mukasa, alisema kamati yake inaishauri serikali kutenga fedha za ndani ili kudhibiti Ukimwi kwa wananchi wake badala ya kutegemea fedha za wafadhili.

# Simanjiro yajitosa kujenga masoko mawili ya madini

**Na Mwandishi Wetu,**
SIMANJIRO

MKOA wa kimadini wa Simanjiro unatarajia kuwa na masoko mawili ya madini ya vito kwenye miji midogo ya Mirerani na Orkesumet kwa lengo la kuteketeza agizo la Rais John Magufuli.

Rais Magufuli aliagiza kujengwa masoko kila ya madini kwa kila mkoa ili kukabiliana na utoshaji wa mali hizo.

Ofisa madini mkazi wa kimkoa wa kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, alisema hayo jana wakati akizungumzia uanzishwaji wa masoko hayo.

Aliongeza kuwa kwa utaratibu wa serikali hivi sasa angalau kila mkoa unatakiwa uwe na soko moja la madini, lakini kwa jiografia ya Simanjiro inapaswa kuwapo na masoko mawili tofauti.

Alisema soko moja litakuwa katika mji mdogo wa Mirerani ambalo litakuwa maalum kwa ajili ya madini ya tanzanite na madini mengine ya vito.

Alisema kutokana na umbali wa kilomita 120 kutoka Mirerani hadi Orkesumet makao makuu ya wilaya hiyo, watajenga soko lingine sehemu hiyo.

"Wafanyabiashara wa madini ya vito ya rubi, green na mengine watatumia soko hilo la Orkesumet na kurahisisha uuzwaji wa madini katika mkoa wetu wa kimadini wa Simanjiro," alisema.

Alisema soko la Orkesumet litawawezesha wafanyabiashara wa madini ya rubi wa machimbo ya Kitwai na Green kwa wachimbaji wa Namalulu na Nadonjukin kuuza madini yao katika soko hilo.

"Wafanyabiashara wa madini ya green wa Landanai na Lemshuku watajiamulia wenyewe kuuza popote watakapopenda watakapoona ni karibu kati ya Mirerani na Orkesumet," alisema.

Alisema kwa vile Mkoa wa Manyara una mikoa miwili ya kimadini ya Simanjiro na Manyara, wenyewe wameona wafanikishe uwepo wa masoko hayo mawili ya madini Mirerani na Orkesumet.

Mfanyabiashara wa madini ya green wa Landanai, James Laizer, alisema uwepo wa masoko hayo utafanikisha uchumi wa wafanyabiashara wa maeneo hayo.

"Kuwapo masoko hayo ni hatua nzuri kwani kila mtu ataamua mwenyewe kutumia soko atakaloona lipo karibu kati ya Mirerani na Orkesumet," alisema.



Mkuu wa wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Elizabeth Kitundu (wa tatu kushoto), akikagua mradi wa maji wenye thamani ya Sh. milioni 210, uliofadhiliwa na mashirika ya Water Aid, Habitat for Humanity na wananchi na baadaye kuweka jiwe la msingi kwenye Kijiji cha Sangara, Kata ya Riroda juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Sido kukamilisha majengo ya viwanda

**Na Mwandishi Wetu,**
BABATI

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo Nchini, (Sido), limeanza kujenga majengo kwa ajili ya viwanda vipya vinavyojengwa maeneo mbalimbali nchini kwa fedha zilizotolewa na Rais John Magufuli ili kuwawezesha wajasiriamali wadogo wanaohitaji maeneo ya kuwekeza viwanda.

Fedha hizo za kujenga majengo ya viwanda zilitolewa mwaka jana kiasi cha Sh. bilioni 5 ambapo kwa Mkoa wa Manyara zimetumika zaidi ya Sh. milioni 777 kwa kujenga majengo matatu ya viwanda katika mji wa Babati.

Majengo hayo yamejengwa na Shirika la Uchumi na Maendeleo la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) na tayari yamekamilika na kukabidhiwa juzi mjini Babati.

Akikabidhi majengo hayo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Sido nchini, Profesa Sylvester Mpanduji, Meneja wa SUMA JKT Kanda ya Kaskazini, Meja Daudi Zengo, alisema mradi huo wa majengo ya viwanda ni wa kipekee nchini.

Meja Zengo alisema mradi huo umekamilika kwa wakati hivyo wanayo furaha ya kukamikisha kama walivyoahidi.

Profesa Mpanduji alisema tayari kuna baadhi ya wajasiriamali wamejitokeza kutaka kuwekeza viwanda vyao kwenye majengo hayo.

Alisema lengo la kufanikisha Tanzania ya uchumi wa kati litafanikisha kutokana na fursa kama hizo zinazotayarishwa.

Meneja wa Sido Mkoa wa Manyara, Abel Mapunda, alisema kukamilika kwa majengo hayo ya viwanda kutaleta mabadiliko chanya ya kiuchumi kwa wajasiriamali wa mkoa huo.

Aliwataka wajasiriamali wa mkoa huo kuchangamkia fursa hiyo kwa kuwekeza mkoani humo kwa lengo la kuongeza tija.

Mkazi wa mtaa wa Nyungu mjini Babati ambaye ni mjasiriamali wa zao la alizeti, Mariam Hamis, alisema hatua hiyo ni kubwa kwenye maendeleo ya wananchi wa Manyara.

Mikoa mingine nchini inayojenga majengo ya viwanda kwa ajili ya wajasiriamli kutokana na fedha zilizotolewa na Rais Magufuli ni Dodoma, Kagera na Geita.

# Barabara ya lami kuunganisha wilaya mbili yaja

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKALA wa Barabara Mkoa wa Manyara, umesema ujenzi wa daraja la kisasa katika kijiji cha Magara utakapokamilika, hatua itakayofuata ni ujenzi wa barabara ya lami itakayounganisha wilaya mbili za Babati na Mbulu.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake meneja wa (Tanroads), mkoani hapa, Mhandisi Bashir Rwesingisa, alisema wanaendelea vizuri na ujenzi wa daraja la Mto Magara ambalo linajengwa na kampuni ya China Railway Severth Group (CRSG).

"Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huo wa ujenzi wa daraja lenye urefu wa mita 84.5 ni pamoja na kujenga barabara unganishi kilometa 4.9 ambapo awali tulitegemea iwe na urefu wa kilometa nne lakini kutokana na maboresho ya usanifu imeonekana ili ikidhi inapaswa iwe na urefu wa kilometa 4.9 kati ya hizo zipo zitakazojengwa kwa lami na zingine changarawe," alisema.

Aidha alisema taratibu zinafanyika kuona kama kilometa zote zinaweza kujengwa kwa kiwango cha lami ili wananchi wa eneo hilo waweze kunufaika na ujenzi wa daraja lakini pia wapate barabara iliyo nzuri ya kuinua uchumi wao. Meneja huyo alifafanua kuwa kazi ambazo wameishazifanya mpaka sasa ni ujenzi wa barabara unganishi kilometa 2.2, kusimika ardhini nguzo 70, kuinua nguzo mbili na kinachosubiriwa ni vyuma na kuweka zege.

Mhandisi Rwesingisa aliiambia Nipashe kuwa ujenzi wa daraja hilo utagharimu Sh. bilioni 12.641 na mpaka sasa mkandarasi ameishajenga daraja hilo kwa asilimia 45 hivyo ifikapo Oktoba, mwaka huu, wanategemea magari yataanza kupita juu ya daraja hilo.

Mkazi wa kijiji hicho, Hadija Abdallah, akizungumzia ujenzi huo alisema Tanroads wakikamilisha daraja hilo watawaondolea adha wazazi ya kuwasindikiza watoto wao kwenda shule kipindi cha masika ili wawavushe mto maana unakuwa umejaa.

Mkazi mwingine, Hamis Ally, alisema kujengwa kwa daraja hilo ni jambo jema kwa wakazi wa eneo hilo kwa kuwa litakuwa kichocheo cha kukua kwa uchumi.

Kwa upande wake, John Chichi, alisema kujengwa kwa daraja hilo kutawasaidia kufanya biashara zao kati ya wilaya ya Babati na Mbulu kwa kuvusha mazao yao lakini kutafungua fursa mpya za kiuchumi ambazo zitakuwa na tija kwa mwananchi mmoja mmoja, wilaya, mkoa na taifa.

# Mkakati kabambe wasukwa kukabiliana ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro, imesema itatumia mpango mkakati wa Wilaya ya Hai kwa ajili ya kutatua matatizo ya mkoa huo yanayohusu matukio ya ukatili zikiwamo mimba za utotoni, ubakaji na ulawiti kwa watoto.

Katibu Tawala wa mkoa wa Kilimanjaro (RAS), Mhandisi Aisha Amour amesema ofisi yake inaunga mkono juhudi zilizochukuliwa na Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya kuunda kamati maalum ya kushughulikia ulinzi wa watoto.

Alikuwa akizungumza jana katika kikao cha wadau wa elimu cha kujadili mpango mkakati wa kutokomeza mimba za utotoni na ubakaji katika Wilaya ya Hai.

Kikao hicho kimewahusisha walimu wa Shule za Msingi 129, Sekondari 43 na Waratibu wa Elimu ngazi ya Kata wapatao 17.

"Kama serikali ngazi ya mkoa tumekubaliana , tutatumia mpango mkakati wa Wilaya ya Hai pamoja na mbinu zinazotumiwa na kamati maalum iliyoundwa na DC Hai (Mkuu wa Wilaya) lakini katika matukio haya yanayoendelea walimu wanahusishwa,"alisema Mhandisi Aisha

Alisema kama mwalimu mwenyewe hataweza kujiheshimu na wazazi wakashindwa kufanya vivyo hivyo, ni wazi kuwa mwanafunzi hawezi kujifunza kwao.

Kutokana na tatizo hilo, Katibu Tawala huyo wa mkoa alionya kuwa ikiwa mwalimu yeyote atabainika au kutiwa hatiani kwa kupewa mamlaka ya kukaa na wanafunzi na yeye kushindwa kutekeleza jukumu lake la ulinzi wa watoto na kuuharibu, wanajua kituo kitakachofuata ni kipi. Kabla ya Mhandisi Aisha kutoa ahadi hiyo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai, Upendo Wella alisema dhumuni la kuitishwa kwa kikao hicho linatokana na kukithiri kwa matukio ya ukatili katika wilaya hiyo ikiwamo mimba za utotoni, ubakaji na ulawiti dhidi ya watoto.

"Inaonyesha matukio yaliyoongezeka ni zaidi ya 20 katika wilaya yetu kwa kipindi kifupi. Mheshimiwa DC aliunda kamati maalum ya kushughulikia tatizo hili na pia kikao hiki kinalenga kukumbushana majukumu yetu, mwisho wa siku tutajipima kwa kile tulichokubaliana,"alieleza Wella.

Wella ameeleza kuwa katika kikao hicho, watatoa maelekezo ya mkakati wa wilaya wa kutokomeza vitendo vya ukatili wa watoto, hali halisi ya ukatili wa watoto katika wilaya na namna ya kuwatambua watoto wenye matatizo.

Aidha, ameeleza kuwa wadau hao pia watautizama wajibu wa mwalimu katika vita hiyo, madhara ya kiafya na kisaikolojia ya kujihusisha na ngono katika umri mdogo, sheria ya mtoto na utoaji wa taarifa na mrejesho kuhusiana na madai au madeni ya walimu.

Awali akiwasilisha mada kuhusu hali halisi ya ukatili wa watoto, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Hai, Salome Zephania, aliwaeleza wadau hao kuwa katika robo ya tatu ya Januari hadi Machi mwaka huu, kumeripotiwa kesi 25 zinazohusu ukatili wa kimwili kwa watoto.



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa kingo za barabara iliyojengwa kwa kiwango cha lami ya Sinza – Tandale, katika eneo la White Inn, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Zaidi ya wafungaji 1,200 wakumbukwa kwa chakula

**Na Godfrey Mushi,** KILIMANJARO

ZAIDI ya wananchi 1,200 jamii ya wafugaji wa kimasai ambao wanaishi katika vitongoji vinne vya Kijiji cha Kambi ya Chokaa katika mpaka kati ya Wilaya ya Simanjiro na Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, wamepatiwa msaada wa vyakula mbalimbali na wasamaria wema kutokana na hali ya ukame kutishia eneo hilo.

Ukame katika eneo hilo unadaiwa kusababisha baadhi ya wafugaji kuhamisha mifugo yao kutokana na kukosa malisho.

Kutokana na hali hiyo, Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Lukani wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Leonard Minja, alisema uamuzi wa kupeleka msaada huo wa ndizi zaidi ya mikungu 700 unatokana na tishio hilo la ukame.

"Kwa muda wa mwezi mmoja sasa, waumini wanaoishi maeneo ya ukanda wa milimani katika Wilaya ya Hai, wamechangia mikungu ya ndizi zaidi ya 700 pamoja na mahindi magunia matano na wanaendelea kuwahamasisha wananchi wa maeneo ya ukanda wa juu wanaolima ndizi kujitolea ili kuzinusuru familia ziliopo maeneo ya tambarare zinazohitaji chakula,"alieleza Mch. Minja

Ameeleza kuwa walipokea wito kutoka kwa Mkuu wa Jimbo la Hai la KKKT, Mch. Aminirabi Swai aliyewataka waumini wa dhehebu hilo waishio ukanda za milimani, ambao wamepata neema ya chakula, kutoa kwa moyo chakula kidogo kwa ajili ya kuwasaidia wenzao waliokumbwa na ukame katika ukanda wa tambarare mpakani mwa Wilaya za Simanjiro na Hai.

"Sharika 10 zilizopo katika ukanda wa milimani wa Wilaya ya Hai, wamejitoa kwa moyo sana kwa kutoa mahindi gunia tano, maharage na ndizi zaidi ya mikungu 700. Sharika hizo ni Sufi, Nsongoro, Lukani, Ng'uni, Kyuu, Nkwansira, Lemira Kati, Ngaya, Mafeeto na Muroma,"alizitaja Mch. Minja

Akizungumzia hali ya ukame inayotishia eneo hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kambi ya Chokaa, Nderiso Ratoi alisema kwa sasa hali ya wananchi ni mbaya kutokana na mazao yao mengi kukauka kutokana na kuchelewa kunyesha kwa mvua za masika.

Pia, baadhi ya wakazi wa vitongoji hivyo waliozungumza na Nipashe akiwamo Maria Stephano na Mosomi Marindi, wameeleza kufurahishwa kwao na msaada huo wakisema kuwa utawasaidia kupunguza makali ya hali waliyonayo hasa kutokana na mazao kushindwa kuhimili ukame.

Kwa upande wake, Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Nomeuti wa KKKT, Mch. Fredrick Minja alisema kuwa usharika wake uko eneo la tambarare na usharika huo una mitaa mitatu ambayo kiserikali imegawanyika katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro na mwingine uko Wilaya ya Simanjiro mkoa wa Manyara.

# EAC yashindwa kutekeleza ahadi yake

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

JUMUIYA ya Afrika ya Mashariki (EAC), mpaka sasa haijaweza kutenga ruzuku kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi ambacho kiliibuka kidedea katika mashindano ya nchi wanachama wa jumuiya hiyo na kutangazwa kuwa kituo mahiri cha mafunzo ya ushirika na biashara katika ukanda huo.

Aliyekuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Prof. Faustine Bee (sasa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma), amedai hayo akisema baada ya ushindi wao mwaka 2013, walipewa ngao na Jumuiya ilitakiwa ianze kutenga bajeti ya kukisaidia chuo kama kituo mahiri cha mafunzo ya ushirika na biashara lakini jambo hilo hadi sasa halijafanyika.

"Licha ya kutakiwa kutoa ruzuku hiyo kama mshindi lakini vile vile ilitakiwa kuwajibika kama jumuiya kuleta wanafunzi na kukitumia chuo, jambo ambalo halijafanyika lakini kutambuliwa huko ni hatua muhimu,"alieleza Profesa Bee

Chuo hicho Kikuu cha Ushirika Moshi ni tofauti na vyuo vingine ambavyo viko katika Afrika ambavyo vyenyewe vina idara peke yake, kurugenzi au taasisi zinazotoa elimu ya ushirika.

Kwa mujibu wa Prof. Bee, hakuna chuo kingine Afrika ambacho kimezamia kwenye elimu ya ushirika zaidi ya vyuo viwili vya Afrika ya Mashariki vya Kenya na Tanzania katika sekta ya ushirika.

Zaidi alisisitiza: "Ninaondoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, nikiwa nakumbuka kwamba mwaka 2013, tulipoingia katika kushindanishwa na Taasisi nyingine za Elimu ya Juu, chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), tulitawazwa kuwa kinara kwa kuwa kituo pekee katika nchi za Afrika ya Mashariki cha Centres of Exllence (kituo cha umahiri)." Profesa Bee, amekuwa mtumishi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kwa miaka 31 sasa na alifanya kazi ya kufundisha, kufanya utafiti lakini pia ameshiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chuo hicho tangu kilipokuwa Chuo cha Ushirika Moshi, baadae Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi na sasa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

Mkuu wa chuo hicho kwa sasa ni Spika wa zamani wa Bunge la Tanzania, Pius Msekwa ambaye pia ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST).





Meneja mradi wa shirika la International Aid Services (IAS), Allan Kamnde (aliyesimama kulia), akitoa mada katika semina ya wadau wa elimu jumuishi katika wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. Shirika hilo, linakusudia kujenga vyumba viwili vya kupima aina ya ulemavu katika wilaya hiyo na Bahi mkoani humo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Rais Magufuli kufungua mkutano wa 35 wa ALAT

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS John Magufuli, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mkutano mkuu wa 35 wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT) utakaofanyika Jijini Mwanza mwezi Juni mwaka huu.

Hayo yalibainishwa jijini hapa jana na mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Gullamhafeez Mukadam, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati akikagua ujenzi wa jengo la ofisi za ALAT makao makuu.

Alisema kaulimbiu katika mkutano mkuu wa 35 wa jumuiya hiyo mwaka huu imejikita katika kuchochea maendeleo ya uchumi pamoja na uboreshaji wa viwanda nchini.

Alisema agenda za mkutano huo ni pamoja na kujadili mafanikio ya ALAT katika utekelezaji wa shughuli kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Juni 2019 na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

"Mkutano mkuu wa mwaka huu utakuwa ni wa aina yake kwasababu utaenda sambamba na utoaji wa Tuzo kwa halmashauri zinazofanya vizuri pamoja na wadau mbalimbali katika utoaji wa huduma na maendeleo ya wananchi kwa ujumla"alisema.

Aidha alisema pamoja na agenda za mkutano mkuu kutakuwa na maonyesho ya bidhaa na huduma mbalimbali zinazotolewa na wadau wa mamlaka za serikali za mitaa nchini.

Vilevile sekta binafsi, Taasisi za serikali na mashirika ya Umma yatashiriki pamoja na viongozi na watendaji wa serikali za mitaa kujadili kwa pamoja masula yenye manufaa kwa pande zote.

Alisema mkutano huo pia utahudhuriwa na Wizara , Idara za serikai kuu, Wakala wa serikali, Taasisi shirikishi katika serikali za mitaa, Makatibu tawala wasaidizi wa mikoa wanaohudumia serikali za mitaa, wawakilishi wa balozi na wadau wa maendeleo, Mashirika ya kimataifa na jumuiya za serikali za mitaa za Afrika na wadau wengine wa sekta za serikali za mitaa.

Aidha mukutano huo pia utahudhuriwa na Asasi zisizo za kiserikali , mashirika na kampuni na wawakilishi wa sekta binafsi ambapo inatarajiwa kuwa mkutano huo kuwa na washiriki takribani 600.

Aidha mwenyekiti huyo akizungumzia ujenzi wa jengo la ofisi ya jumuiya hiyo unaoendelea jijini hapa alisema kuwa kwa miaka 35 toka kuanzishwa kwa ALAT haikuwahi kuwa na jengo kama hilo.

"Miaka 35 ya ALAT leo hii tunafanya mageuzi kwa kuwa na jengo la ofisi katika makao makuu ya nchi jambo ambalo lilishindikana kwa miaka yote iliyopita" alisema

Hatahivyo alisema jengo hilo ni la muda kwa kua hivi sasa tayari wameshachora ramani yenye ghorofa nane ambayo wanatarajia ujenzi wake kuanza mara baada ya mkutano mkuu ili kuwa na kitega uchumi kitacho wawezesha katika kutatua changamoto mbalimbali.

# Utafiti wabaini mazito miundombinu ya wanafunzi

**Na Elisante John,** SINGIDA

UTAFITI uliofanywa kwa shule za msingi na sekondari katika halmashauri ya wilaya Singida na Chamwino Mkoani Dodoma, umebaini ushiriki duni wa jamii katika elimu umechangia miundombinu isiyo rafiki kwa wanafunzi.

Hayo yalielezwa juzi na Joachim Muyawani kutoka Asasi ya BLUWAT, iliyofanya utafiti huo mkoni Singida chini ya shirika la Action Aid, kwa ufadhili wa Shirika la Ushirikiano na Maendeleo la Nchini Norway (NORAD).

Alisema kuwa tatizo hilo ni kubwa kwa wanafunzi, hasa walemavu waliopo kwenye shule zilizopo maeneo ya vijijini hali inayosababisha wajifunze huku wakiwa kwenye mazingira yasiyo rafiki katika kupata elimu. Kwa mujibu wa Muyawani, utafiti huo ulijikita katika miundombinu na mazingira, ikiwemo ile ya wanafunzi kujisomea, vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo kwa wanafunzi na walimu, nyumba za walimu na wingi wa wanafunzi darasani.

Aidha, utafiti huo ulihusisha miundombinu ya wanafunzi walemavu, ambayo hata hivyo ilielezwa kuwa shule nyingi hazijajengwa ngazi mterezo kwa ajili ya walemavu, huku vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa wasioona na wenye uoni hafifu, vikikosekana katika shule.

Kutokana na hali hiyo Muyawani, aliitaka jamii kushirikiana vema na serikali katika kuiboresha miundombinu hiyo ili kufikia lengo lililokusudiwa na serikali la elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi sekondari.

Alifafanua kuwa haki ya wanafunzi kujieleza bado ni tatizo kwenye shule nyingi, huku unyanyasaji (ukatili) dhidi ya wanafunzi likizidi kuwa tishio, pia haki ya kujieleza bado zipo chini, huku hali ya uwazi katika bajeti ikionekana ya kuridhisha.

Naye mwakilishi wa Shirika la Maendeleo na Elimu Mtinko (MEDO), Hassan Rasuli, alisema ni muhimu kwa jamii kushiriki kazi za kijamii ambazo zinahusisha makundi maalumu ili kuvunja vikwazo vilivyopo.

Rasuli alisema kuwa jamii inapaswa kupokea kwa usahihi sera ya serikali ya awamu ya tano kuhusu elimu bure, kwa kushirikiana na serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo, lengo likiwa ni kumaliza kabisa kero zinazoikabili sekta ya elimu hapa nchini.

Mwakilishi huyo kutoka MEDO, alisema kuwa, utafiti huo ulihusisha jumla ya shule 20, ikiwa ni kumi kutoka katika wilaya hizo mbili zilizofanyiwa uchunguzi, zikiwemo saba za msingi na shule tatu za sekondari, kwa kila halmashauri zote mbili, Chamwino na Singida

# Shirika kujenga vituo kupima aina ya ulemavu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SHIRIKA lisilo la Kiserikali la International Aid Services (IAS), linatarajia kujenga vituo viwili vya kupima na kufanya utambuzi wa aina ya ulemavu kwa wanafunzi wenye ulemavu katika wilaya mbili mkoani hapa.

Hayo yalielezwa na meneja mradi wa shirika hilo hapa nchini, Allan Kamnde, wakati alipokuwa akizungumza kwenye semina ya wadau wa elimu jumuishi iliyofanyika wilayani Chamwino mkoani hapa jana.

Kamnde alisema shirika hilo linatarajia kujenga miundombinu ya majengo na vituo viwili vya kupima aina ya ulemavu kwa wanafunzi wenye ulemavu wanaosoma na wanaokusudia kusoma katika shule mbili zitakazopendekezwa na uongozi wa Wilaya ya Bahi na Chamwino.

Alisema lengo la shirika hilo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kutoa elimu kwa watoto wenye ulemavu nchini kupitia utaratibu wa elimu jumuishi, ambao unamwezesha mtoto mwenye ulemavu kuipata katika maeneo ya karibu na anapoishi. Meneja huyo alisema shirika hilo litakuwa tayari kujenga vituo hivyo vya mfano katika shule moja kila wilaya ili kuweza kuwasaidia wanafunzi hao wenye ulemavu kupata elimu.

Alisema katika shule itakayopendekezwa shirika hilo litajenga mindombinu ya njia kwenye majengo na njia wanazotumia wanafunzi walemavu shuleni pamoja na jengo moja la kuweka vifaa vya kufanyia vipimo.

Alibainisha kuwa kwa sasa shirika linaendelea kutoa elimu na semina kwa makundi ya wazazi, wanafunzi , waalimu na viongozi wa ngazi ya wilaya kabla ya kuonyeshwa shule watakazotakiwa kutengeneza miundombinu hiyo kwa ajili ya walemavu.


Alisema vituo hivyo vitakuwa na uwezo wa kupima aina ya ulemavu alionao mtoto na kutambua ili kumsaidia kwenye masomo yake akiwa shuleni na walimu wanaowafundisha.

"Kuna wakati mwingine mwalimu anaweza kumuuliza swali mwanafunzi darasani na mwanafunzi akabaki anamwangalia tu, na mwalimu bila kujua akachukua hatua ya kumwadhibu kumbe mwanafunzi huyo ni kiziwi hivyo kupitia mafunzo haya tunasaidia kuwaelimisha" alisema. Kamnde alisema Shirika hilo linafanya kazi katika mikoa ya Rukwa, Katavi na Singida na hivi karibuni wataanza ujenzi kwenye Makao makuu ya nchi kwa wilaya hizo mbili.

Aidha, alisema elimu jumuishi ni utaratibu wa upatikanaji elimu kwa watoto wote bila kujali hali ya ulemavu , kiuchumi, kidini , rangi au kabila , jinsia , wote wanapata elimu bila kubaguliwa.

Aliongeza kuwa vituo hivyo vitakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo husika pamoja na yale ya jirani hata nje ya mkoa husika.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Buigiri, Keneth Yindi alisema kama uongozi wa Wilaya ya Chamwino watachagua miongoni mwa shule ya kata yake kuwapo kwenye mpango huo, wananchi watakuwa tayari kutoa nguvu kazi ili kufanikisha malengo ya ujenzi wa kituo hicho.





# Samia awataka Wazanzibar kuenzi fikra za hayati Karume

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassani amewataka wananchi wa Zanzibar kuenzi na kudumisha fikra za maendeleo za kiuchumi, kisiasa na kijamii za hayati Sheikh Abeid Amani Karume kwa vitendo.

Alisema fikra hizo za maendeleo katika upande wa kiuchumi wananchi wanapaswa kuzidumisha kwa vitendo kwa kuhakikisha rasilimali za nchi zinalindwa kwa kuwa Rais Karume alikuwa anazilinda.

Akifungua kongamano la pili la kumbukumbu ya Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, alisema fikra hizo zilikuwa zina lengo la kondoa dhuluma walizokuwa wanafanyiwa Wazanzibar.

Samia alielea kuwa kwa upande wa fikra za kijamii inapaswa kuziendeleza kwa kutoa huduma bure katika sekta ya elimu na afya kama alivyotangaza katika kipindi cha mwaka 1964.

"Rais Karume pia aliamini katika misimamo ya fikra za kuwaunganisha Wazanzibar katika nyanja ya kisiasa ambapo baada ya mapinduzi kufaulu aliondoa mfumo wa vyama vya siasa na kuanzisha mfumo wa chama kimoja kwa lengo la kuondoa ubaguzi kati yetu," alisema Makamu huyo wa Rais.

Alisema, Rais Karume alikuwa na fikra za kuleta hali ya umoja, utu na heshima kwa Wanzanzibar na alikuwa kiongozi ambaye anakemea vitendo vya dhuluma ambapo alihakikisha kila mwananchi anapata haki sawa. "Rais Karume alihimiza umoja na muungano wetu hivyo tunatakiwa tuenzi kwa vitendo kwa kuimarisha muungano ulioko lakini pia alikuwa hana maamuzi ya pekee yake bali yeye alikuwa ana shauriana na Baraza la Mapinduzi na Baraza la wazee la ASP na inavyosemekana alikuwa anakutananao mara kwa mara ofisi ya chama Kisiwandui,"alisema.

Makamu huyo wa Rais alisema anapongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar(SMZ), inayoongozwa na Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kuendeleza kwa vitendo fikra hizo ikiwamo utoaji wa huduma za elimu bure na afya.

Mapema akimkaribisha Makamu wa Rais, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Mwalimu Nyerere, Steven Wasira, alisema lengo la kongamano hilo ni kuenzi fikra na falsafa ya kiongozi huyo wa kwanza wa Zanzibar.

"Kongamano hilo ni la makusudi kumuenzi na kumtukuza kwa kile alichokifanywa kwa kupigania na kuleta maendeleo ya Zanzibar kwa ujumla,"alisema Wasira.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema fikra za Hayati Rais Karume bado zinapaswa kuheshimiwa kutokana na kuwa zina lengo la kuheshimu utu na uhuru Wazanzibar.

Alisema kuwa Rais Karume alikuwa na dhamira ya kuendeleza maendeleo ya Zanzibar ambapo katika kipindi cha mwaka 1970 hadi 1975, alijenga majengo 72 ya ghorofa kwa kipindi cha miaka mitano tu na kwamba hali hiyo ni ishara ya fikra za maendeleo katika nyanja ya kijamii.

"Hii inaonesha kuwa Rais Karume alikuwa mtu wa kutekeleza fikra za maendeleo kwa wakati na kwa tija ya wazanzibar wote hivyo lazima tuhakikishe tunamuenzi kwa vitendo fikra zake,"alisema Mkuu huyo wa Mkoa



Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mohamed Ahmada (wa tatu kushoto), akikabidhi cheti kwa mteja wa benki ya NMB Zanzibar, Mrisho Haji, kwenye kongamano la Klabu ya Biashara iliyoandaliwa na benki hiyo na kuhudhuriwa na wafanyabiashara zaidi ya 300, mjini Zanzibar juzi. Wengine pichani ni viongozi wa klabu ya wafanyabiashara Zanzibar na wafanyakazi wa NMB. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtumishi ZEC adaiwa kumpachika mimba mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, linamshikilia mfanyakazi wa Tume ya Uchaguzi (ZEC), Abdalla Juma Abdalla (45), kwa tuhuma za kumpa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha tatu na kumuingilia kinyume na maumbile.

Hayo yamethibitishwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo Tobias Sedayoka alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari huko ofisini kwake Madema.

Alisema kuwa mtuhumiwa huyo anadaiwa kutenda makosa hayo kwa mwanafunzi huyo ambae ana umri wa miaka 16 jina tunalihifadhi.

Alisema kuwa tukio hilo liliripotiwa juzi katika ofisi yake na bado mtuhumiwa yupo chini ya ulinzi kwa kuhojiwa.

"Tukio limeletwa hapa Juzi Alhamis lakini mtoto huyo anadaiwa kuwa na ujauzito wa miezi mitatu sasa lakini baya zaidi amemuingilia pia kinyume na maumbile,"alisema.

Hata hivyo alisema kuwa Polisi inaendelea na utaratibu wake wa kufanya uchunguzi na ukikamilika mtuhumiwa atafikishwa kwenye vyombo vya sheria. Kamanda huyo aliwataka wananchi kuendelea kuyaripoti matukio hayo ili wahusika waweze kufikishwa katika vyombo husika na haki kutendeka.

Wakati huohuo, kamanda huyo akizungumzia kumbukumbu ya Mzee Karume, rais wa kwanza wa Zanzibar aliwatahadharisha wale wote ambao wanahudhuria katika dua ya kiongozi huyo wakiwa wamelewa .

Alisema sehemu ya dua hiyo sio sehemu ya kufanya vurugu au vitendo visivyo na maadili na atakaehudhuria katika dua hiyo akiwa amelewa hatoruhusiwa kuhudhuria katika dua hiyo.

"Wapo baadhi ya watu huja katika dua hii huwa wameshalewa kwa hivyo tunawaambia wakae hukohuko majumbani mwao"alisema.

Dua hiyo ya kumbukumbu ya mzee Karume inatarajiwa kusoma kesho jumapili ambapo itahudhuriwa na viongozi mbalimbali inatarajiwa kufanyika ofisi kuu ya CCM kisiwandui.

# Wawekezaji waonywa kufuata sheria

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAWEKEZAJI wametakiwa kuheshimu na kufuata sheria za nchi wanapoanzisha miradi yao ili kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza ikiwamo kusitishwa shughuli za kazi wanazozifanya.

Hayo yameelezwa na Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar, Khamis Mwinyi wakati akizungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar, baada ya kupokea malalamiko ya wafanyakazi wa kampuni ya ulinzi ya Kenya (KK SECURTY) kwa kutolipwa mishara yao kisheria.

Alisema kuna baadhi ya wawekezaji wamekuwa wakikiuka sheria na taratibu za nchi jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya mikataba yao.

Alisema kampuni za KK Securty imekuwa ikilalamikiwa sana na wafanya kazi wake kwa kuwakosesha haki zao za msingi ikiwamo kutowalipa mishahara iliyotangazwa na serikali pamoja na kukwepa kulipa malimbikizo ya madeni hao.

Alieleza kuwa serikali imetangaza kima cha chini cha mishahara ni Sh. laki tatu lakini kampuni hiyo haijatekeleza ahadi hiyo. Alisema licha ya serikali kutangaza kima hicho lakini bado kuna baadhi ya taasisi hazifuati agizo hilo ikiwemo kampuni ya ulinzi ya KK Securty jambo ambalo ni kukiuka sheria na taratibu za nchi pamoja na kupinga agizo la Raisi wa Zanzibar.

Alisema ni vyema kwa kampuni hiyo kuandaa utaratibu wa kuwalipaa wafanyakazi wake ili kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza ikiwamo kuchukuliwa hatua za kisheria.

Aidha, Katibu huyo alitoa wito kwa taasisi zinazosimamia masuala ya ajira kuendelea kufuatilia agizo la serikali juu ya utekelezaji wa mishahara kwa taasisi binafsi ili wafanyakazi waweze kunufaika na haki zao za msingi ikiwamo kulipwa mishahara inayoendana na kazi wanazofanya.


Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa chama hicho, Rihi Haji Ali, alisema wameshafanya juhudi mbalimbali za kukaa na kampuni hiyo lakini bado imekuwa haitaki kufuata sheria za kazi.

Alisema zaidi ya vikao vitano wameshakaa chama cha wafanyakazi pamoja na uongozi wa kampuni hiyo lakini hawaoneshi matumaini ya kuyafanyia kazi mazungumzo yanyozungumzwa katika vikao hivyo.

Alisema ni vyema kwa serikali kuunga mkono juhudi za chama hicho katika kutatua matatizo yanayowakabili wafanyakazi wa kampuni hiyo.

Aidha, alisema mbali na kampuni hiyo pia watahakikisha wanafatilia kwa undani taasisi nyingine ili kuibua matatizo yanayowakabili wafanyakazi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI APRILI 6, 2019



**KHEE, AMBER LULU KWA UJIKO!**
Soma UK.14




# DIMPOZ

# AFYA KWANZA

## BASI SAWA



## Huo ndio uungwana Bill Nass

NIMESAMEHE. Ni msimamo wa Bill Nass, anapotangaza kumsamehe Steve Nyerere, ingawa hajui chanzo cha ugomvi wao ambao sasa umedumu kwa zaidi ya mwaka mmoja.

"Sijui kwanini amekuwa akinisakama mara kwa mara, lakini nimemsamehe, kwani ninaona kama anatafuta kiki kupitia kwangu," amesema Bill Nass.

Msanii huyo amesema Steve Nyerere hana jambo jipya kwenye filamu, sasa analazimisha ugomvi ili jamii ijue kwamba yupo wakati alishapotea kitambo.



## Khee, Amber Lulu kwa ujiko!

MSANII asiyeishiwa vituko, Amber Lulu, amejifagilia mbaya eti haoni msanii yoyote wa kike anayemfikia katika kujipamba, kuvaa pamba kali na kuvutia mashabiki.

"Katika uvaaji mimi niko vizuri, hao wengine wanafuatia, na sijaona msanii wa kunifikia, kwasababu ninajua jinsi ya kujipamba ili nipendeze," amesema Amber Lulu.

Msanii ni lazima awe mbunifu, na kwamba huwa hachukui nguo na kuvaa tu bali anaangalia kwanza kama inaweza kumkaa vizuri na kuvutia mashabiki wake na ina viwango vikali, anatamba.



## Afya kwanza muziki baadaye-Dimpoz

STAA Ommy Dimpoz, amesema hana mpango wa kurejea jukwaani kwa sasa mpaka madaktari wake watakapojiridhisha na uimara wa afya yake.

Amesema hayo akifafanua kuhusu mikakati yake ya kurudi kwenye gemu baada ya kupata hitilafu ya koo hapo mwaka jana na kuitibiwa nje na ndani ya nchi.

"Bado sijarudi rasmi kwenye majukwaa mbalimbali ya muziki. Najitizamia," amesema.

"Nasubiri vipimo kutoka kwa madaktari watakaotoa ruhusa ya mimi kuanza kuimba ama lah," ameongeza.

Hata hivyo pamoja na kuugua kwake aliachia ngoma zake mbili hivi karibuni zilizofanya mashabiki wake kuona ukuu wa Mungu kupitia mapito aliyopitia, gwiji huyo.

## INSTA-TWITTER





**Eti,** Mlikuwa mnangoja nigeuke?-**Shilole.**



**Rafiki** yangu mwema Biblia niongoze na unifikishe mbinguni salama-**Jini Kabula.**



## Chid Benz naye kama Konki Master

INAONYESHA Kwaresma imekuja na neema kwa wasanii, kwani baada ya msanii Dudu Baya maarufu mama Konki Konki Konki Master kuomba radhi, msanii mwingine wa muziki wa kufokafoka Chid Benz naye ameamua kuwaomba msamaha wote aliowahi kuwakosea hapo awali.

Mkali wa muda mrefu amesema haoni maana ya kuwekeana vinyongo kwani duniani wote ni wa kupita tu.

"Kama kuna mtu yeyote anahisi nimemkwaza na kumkosea, sidhani kama kuna ulazima wa kuwekeana vinyongo," amewasihi.

"Kikubwa ni kusameheana na kuacha maisha yaendelee maisha haya ni mafupi na bifu hazina maana," ameongeza.

Dudu Baya au Konki kama anavyojiita hivi karibuni aliamua kumuomba msamaha kwa familia ya marehemu Rugemarila Mutahaba baada ya kutoa maneno yake ya kuudhi aliyoyatoa mara baada ya Ruge kufariki.

Dudu Baya alikiri kukosea na kumuomba msamaha marehemu Ruge pamoja na ndugu jamaa na marafiki juu ya kauli zake akidai kuwa kipindi hiki cha mfungo wa Kwaresma ni cha toba , tena si muda wa kutunza vinyongo.

UNASEMAAA...

## Eti Kala kakamilika?

RAPA Kala Jeremiah, hatarajii kutungiwa nyimbo na wasanii wengine kwa maelezo kwamba mwenyewe anajitosheleza, kakamilika kwa kila idara.

"Kipaji changu ni kuimba na kutunga, hivyo sina sababu ya kutafuta mtu anitungie, zaidi sana mimi ndio huwa ninatungia wengine," amesema Kala.

Ametamba kuwa hata akishirikishwa katika nyimbo za wasanii wengine hupenda kuweka mashairi yake ili aimbe kwa hisia zaidi kuliko kupewa maneno na mwenye wimbo.



## Nay umechukua uamuzi mzuri

RAPA Ney wa Mitego, ameweka wazi kuwa ameacha mambo ya ubabe akidai yamekuwa yakimfanya akosane na wasanii wenzake mara kwa mara bila sababu.

Hata hivyo, amesema iwapo watamzingua, hatasita kuwapasha kupitia muziki kama ambavyo amekuwa akifanya kupitia nyimbo zake ukiwamo wa 'Shika Adabu Yako'.

"Kwanza ubabe wangu ni wa mikwara tu ila nimeachana na mikwara, lakini wakinichokoza au wakifanya mambo ya ovyo nitakuwa ninawalipua kipitia nyimbo siyo kupigana nao," amesema Nay.



BODA 2 BODA

## Tumaini awaomba Wabongo kura



MWIMBAJI wa muziki wa Injili, Tumaini Msowoya, amewaomba wapenzi wa muziki wake kuendelea kumpigia kura ili ashinde tuzo ya Maranatha inayotolewa nchini Kenya-ikibeba jina la 'Mgwama Awards'.

Msowoya anayetamba video ya 'Nina Furaha' pia ni mwandishi wa habari na mwanaharakati wa haki za watoto na wanawake.

Akizungumza na gazeti hili, anawaomba Watanzania kumpigia kura ashinde tuzo hizo zinazotarajia kutolewa May 22, mwaka huu jijini Nairobi.

Mpaka sasa Msowoya anatamba na video tatu zote zikiwa kwenye ukurasa wake wa 'youtube' zikiendelea kufanya vizuri.'

Amezitaja video hizo kuwa ni 'Hakuna Matata', 'Nina Furaha', na 'Ni Mwema'.

"Nina Furaha ndio wimbo ulionitambulisha zaidi, naomba sana Watanzania wenzangu mnipigie kura niweze kushinda tuzo hii ya kimataifa. Nashindana na watu wa mataifa mbalimbali kura zenu ndizo zitakazonitoa," anasema.

Pamoja na kuitamani tuzo ya Maranatha yupo kazini akiandaa na kukamilisha albamu yake ya video anayotarajia kuingiza sokoni June mwaka huu.

"Albamu ikikamilika nitafanya uzinduzi na natarajia kuiweka wakfu hapahapa Dar es Salaam kisha nitazunguka mikoa mbalimbali kwa ajili ya kuitambulisha," anasisitiza.





@burudanitele

>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Usipende** kuwa mtu wa kulalamika bali kuwa mtu wa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila jambo-**Elizabeth Michael Lulu.**



**Kuku** akitaga yai moja anautangazia ulimwengu mzima, wakati ng'ombe anatoa maziwa kila siku yakutosha kijiji kizima wala hapigi kelele. Jifunze kunyamaza-**Madee Ali.**



**Inabidi** nizigawe zile nguo za zamani zote, maana wiki tu nishapungua hazinitoshi loh. Mazoezi ni afya-**Shetta.**

# Kuumbe!



# ESHA BUHETI
## unatuunguza pua wenzio

**Na Adam Fungamwango**

USTAA si kujisikia, na wala si kujiona kuwa tayari umekuwa mfalme au malkia.

Hata uko Ulaya, mtu akishakuwa staa anakuwa amepata fursa ya kuutumia kwenye kupiga pesa.

Ndiyo maana utakuta wachezaji soka, mpira wa kikapu, au wanamuziki na wacheza filamu pesa zao wanawekeza kwenye biashara nyingine, wakitumia usupastaa wao kuendelea kuingiza pesa kwa njia nyingine.

Hapa Bongo wapo wasanii ambao wao wakishakuwa mastaa, hawautumii vizuri. Na kwa kiasi kikubwa hii inawakumba zaidi wanawake.

Baadhi ya wanawake wakishatoa ngoma na kuanza kujulikana kwenye bongo fleva au kupata nafasi ya kucheza filamu na mitaani kuanza kumfahamu, basi ishakuwa tabu.

Hataki tena kazi nyingine yoyote. Ameshakuwa staa. Kazi ni kuombaomba na kuwafuata watu wenye pesa ambao wengine wanakuwa na masharti ya ajabu ajabu ili kuwawezesha.

Ni ukweli uiopingika kuwa sanaa ya muziki wa bongo fleva au filamu haijawa ya moja kwa moja, kwani msanii anaweza kupata shoo leo, nyingine akaipata baada ya miezi mitatu inategemea pia ni umaarufu wake. Hata wachezaji filamu ni mpaka uitwe kucheza kipande fulani na hii ni mpaka waandaaji waone unafaa kucheza hapo.

Hii inawafanya wasanii hao kwa muda mrefu kuwa nyumbani tu.

Wakati wa kusubiri kazi hasa watoto wa kike, kuna baadhi wanajidhalilisha, lakini wengine wanatumia umaarufu wao kujiingiza kwenye biashara mbalimbali zinazowaingizia pesa.

Mfano ni Esha Buheti. Yeye ni msanii mkubwa wa filamu hapa nchini, lakini akiwa hajapata kazi yoyote ya kwenda kucheza, anajishughulisha na mambo mengine. Ana mgahawa wake, ambao anapika na kuuza chakula, huku pia akiwa na saluni ya kike.

anasema akiwa kama mwanamke mpambanaji, hawezi subiri kuigiza muda wote.

"Kama sipati nafasi ya kuweka uhusika wangu kwenye filamu siwezi kukaa tu na kusubiri kupata hiyo fursa," anasema na kuongeza.

"Kila kitu ni kupangilia ndio maana utaniona kwenye movie, saluni na baadaye kwenye mgahawa wangu," anasema.

Anachofanya Esha ni kupangilia vizuri kazi zilizo mbele yake ili maisha yasonge.

Akipata nafasi anakwenda kucheza filamu, akimaliza hakai tu kusubiri kwa sababu hajui ni muda gani itakaa bila kazi. Anachofanya ni kuendelea na biashara zake alizofungua. Hizi zinamuingizia pesa kwa sababu, ustaa pia unamsaidia kupata wateja lukuki.

Hili ni fundisho kwa baadhi ya wasanii wa kike wote nchini.

Wakati wanapokuwa nje ya kazi zao za usanii watafute vitu vingine vya kuwaingizia kipato badala ya kusubiri kazi zipatikane, kwani zinaweza kuchukua muda mrefu na wao kuathirika kiuchumi. Na mara nyingi wasanii wa kike wanapoathirika kiuchumi wanawapa fursa wanaume wakware kuanza kufuatilia na kuwadhalilisha utu wao kwa kuwashushia heshima mbele za mashabiki wao.





# WALIOUBADILISHA MUZIKI WA DANSI BONGO

**Na Mwandishi Wetu**

MWANZONI mwa miaka ya 2000 kulitokea mageuzi makubwa ya muziki wa dansi wa Tanzania.

Yalitokana na ujio wa bendi ya Wenge Musica mwishoni mwa miaka ya 1990. Wakati walipoondoka kuna kundi jingine la wanamuziki Wacongomani waliokuwa wakiishi nchini waliunda bendi ya Diamond Sound 'Wanakibindankoi' ambao waliiga nyimbo hizo, pamoja kutunga zao ambazo ziliwapatia umaarufu mkubwa.

Wigo uliongezeka baada ya kuundwa bendi pinzani ya FM Musica ambayo nayo iliendeleza muziki huo wenye vionjo hivyo.

Kuona hivyo, wanamuziki wa Kitanzania nao walifanya mageuzi, kwani baadhi walianza kupiga muziki wenye vionjo vya bendi za Congo hasa Wenge Musica na nyingine kama Extra Musica za Koffi Olomide.

Hapo ndipo zilipoanzishwa bendi mbalimbali kama African Stars 'Twanga Pepeta', Mchinga Sound, Chuchu Sound, Mokibo Sound, African Revolution na Akudo Impact.

Wanamuzika hawa, hata hivyo, walitofautiana na wenzao wa Diamond Sound na FM Academia.

Walikuwa wakipiga nyimbo za zenye maneno ya Kiswahili kuanzia tungo mpaka rapu, lakini mapigo ndiyo yalikuwa yakifanana na ya Wakongo.

Kuna wanamuziki wa Kitanzania waliovuma sana kipindi hicho na kuwa mastaa na kuchukuliwa kama wao ndiyo wanamageuzi wa muziki wa dansi wa Kitanzania wenye vionjo vya Kikongo nao ni pamoja na:

**Ramadhani Masanja 'Banza Stone'**

Mwanamuziki huyu haswa anachukuliwa kuwa ni Mtanzania aliyeleta mageuzi ya muziki wa dansi wenye mapigo ya Kikongo kuweka maneno ya Kiswahili mwanzo hadi mwisho.

Alikuwa mmoja wa waasisi wa African Stars 'Twanga Pepeta' na aliipaisha kwa nyimbo kali, uimbaji na rapu ambazo zote alizibadilisha kutoka kwenye lugha ya Kikongo kwenda Kiswahili, ambazo zilimfanya kujikusanyia mashabiki Bara na Zanzibar.

Mbali na Twanga Pepeta, Banza Stone alitamba pia kwenye bendi za TOT Plus, Bambino Sound na African Revolution. Alifariki dunia Julai 17, 2015 jijini Dar es Salaam.

**Ally Choki**

Choki pia ni mmoja wa Watanzania walioleta mageuzi ya muziki wa aina hii. Umaarufu wake ulibanwa kidogo wakati Banza Stone yuko Twanga Pepeta.

Alipoondoka kwenda TOT bendi ya CCM, Choki alichukua usukani na kutunga nyimbo kama 'Jirani', 'Busu la Kufunga Mwaka' na nyingine nyingi zilizompatia jina na kuifanya pia Twanga Pepeta kuwa tishio.

Choki pia kama ilivyo kwa Banza Stone, naye alikwenda TOT Plus, lakini pia alianzisha bendi yake ya Extra Bongo akipiga aina hiyo hiyo ya muziki hadi leo hii.

**Mwinjuma Muumini**

Ni mmoja wa wanamageuzi wa muziki wa Kitanzania ambaye alianza kujulikana akiwa kwenye bendi ya Mchinga Sound. Baada ya kuleta ushindani mkubwa dhidi ya Twanga Pepeta.

Hakuwahi kuipigia bendi hiyo, lakini alichukuliwa na uongozi wa Twanga Pepeta kwenda kuiongoza bendi dada ya African Revolution ambayo iliingia na mtindo wa Tamtam, badala ya Chumvi Chumvi Tutalamba iliokuwepo awali.

**Luiza Mbutu**

Ni mwimbaji mwanamama ambaye alishiriki kuleta mageuzi hayo tena ndiye dada wa wanamuziki wote wa kike wanaoimba muziki wa Kitanzania kwenye vionjo vya Kikongo.

Wimbo wa 'Kisa Cha Mpemba' aliouimba na Banza Stone', ukiwa wa kwanza kuchomoza na kuleta mapinduzi makubwa ya muziki wa aina hiyo nchini, ulimfanya binafsi kuwa maarufu hadi leo hii.

**Hadija Mnoga 'Kimobitel'**

Baada ya Luiza Mbutu ambaye awali kabla ya kuolewa alijulikana kama Luiza Nyoni, aliibuka mwanadada mwingine mwenye sauti tamu na akachukua umaarufu mkubwa akipitia bendi mbalimbali kama Twanga Pepeta, Tamtam, Extra Bongo na nyingine nyingi, ni Hadija Mnoga.

Kimobiteli alikuwa chachu ya muziki wa aina hii kuzidi kujiongezea umaarufu mkubwa nchini kabla ya kufifia kwenye miaka ya hivi karibuni.

Banza Stone



Ally Choki



Mwinjuma Muumini



Luiza Mbutu



Kimobitel

# Vijimambo

## PICHA ILIYOPITA



1. Mbona kama sielewi. Picha niliyopiga iko wapi? - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Mshaanza kunijadili, Watanzania bwaaana! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
3. Hii kazi ya upaparazi itaniua. Maana kufuatilia siri za chui si mchezo - Mama Nah, Manzese.
4. Daah, betri imeshaisha chaji sijui nafanya nini sasa - Ndulu James, Sinza DSM.
5. Hii sasa ndio picha. Simba kaliwa na swala, si mchezo - Beneali Mouusa, Migombani Zenji.
6. Napiga picha kwa maharusi tu - Shirima, Morogoro.
7. Wewe jifanya tu unajua kupiga picha, simba nao wanakuvizia ujue - Dachi G. Dachi, Dodoma.
8. Badala ya kunitea ndizi, wameniletea hiki kidubwasha, sasa nakifanyia nini? - Moussa Beneali, Zenji.
9. Oook! Sasa nimeelewa namna ya kuitumia hii kitu - Nuru Msagusa, Masiwani Tanga.
10. Lazima nimtoe huyu mwenzangu humu ndani. Sijui hata walimuingizaje - Baruli Msagusa, Tanga.
11. Acha kushangaa wewe, njoo huku mjini utuuzie, huwezi kuitumia hiyo - Mama Nah, Manzese DSM.
12. Cha kuokota si cha kuiba, sasa ngoja atokee mtu ajifanye yake. Namkata makofi - Mariam Beneali, Zenji.
13. Hiki kweli kinaliwa jamani? Mbona sioni mahali pa kufungua wala kumenya? - Digos Juma, Buguruni DSM.
14. Yeeah baba, hii picha imetoka safi saaana! - Mr. H., Segerea DSM.
15. Hawa watu humu ndani mbona hawanitupii ndizi? Nitawatoa! - Baba Juma, Kunduchi Mtongani.
16. Mara paaa, mzee baba kaokota kamera, porini watajuta! - Baba Juma, Kunduchi Mtongani.
17. Nirekebishe kwanza, nikipiga kitu bomba - Mama Collin, Ruvuma Kwa Matco.
18. Duuuh, hatari kama fundi vile! - Ali, Bigwa.
19. Picha hizi napeleka Idara ya Habari - Mfaumbe Mbugi, Mshindo Iringa.
20. Ngoja nifanye 'photo shop' ili nipake 'like' na komenti insta. Mitandao inatupelekesha! - Agatha Mbale, Moro Town.
21. Babulai usihamishe pozi, naseti kamera - John Kivuyo, Arusha.


**SMS Bomba ya Leo:**

**Hiki kweli kinaliwa jamani? Mbona sioni mahali pa kufungua wala kumenya? - Digos Juma, Buguruni DSM.**

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Ushirikina ulivyosambaratisha familia

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kwamba ina ucheshi mkubwa, lakini filamu hii inatoa fundisho kwa wale wote wenye tabia ya kuhukumu wenzao kwa kudhani kuwa wametenda hatia fulani.

Kudhania ni jambo mbaya. Ndiyo maana sheria za jinai inataka upande wa ulalamikaji uwe na ushahidi usiotia shaka ili kumhukumu mshtakiwa pasipo hofu wala fikira za kumuonea.

Ni bora uwaachie watu 10 waliofanya makosa, kuliko kumfunga mshtakiwa mmoja kwa ushahidi wa kuzua na kuungaunga.

Filamu hii ya 'Mama Mwali' pia inaifundisha jamii kuwa ushirikina haufai, kwani ni udanganyifu tena ni imani za kufikirika, lakini pia unaweza kusababisha madhara na kusambaratisha jamii kutokana na masharti magumu, anayopewa mteja anapowazuru masangoma.

Imechezwa na Muhogo Mchungu, Koleta Mkemangwa, Madebe Lidai, Sabrina Marijani, Juma Fimbo na wengineo.

Inaanza kwa Mama Sikujua kwenda nyumbani kwa kijana Fimbo kumsemea mbovu kwa madai kuwa anatembea na binti yake.

Baada ya kutomkuta binti yake, Mama Sikujua anaondoka na kukutana na ndugu yake Fimbo aitwaye Mpumbavu.

Anamueleza yote anayoyafanya kaka yake kisha Mpumbavu anakwenda nyumbani kwa Fimbo na kumwambia kama anampenda Sikujua basi afuate taratibu zinazotakiwa, ikiwa ni pamoja na kupeleka barua na kuoa.

Fimbo anafanya kama alivyoagizwa na Mpumbavu. Barua inapelekwa, Sikujua anawekwa ndani, ni mwali kwa ajili ya kufundwa, tayari kwa kuolewa.

Dada yake Sikujua aitwaye Siwajibu bila aibu anamfuata Fimbo na kumweleza shemeji yake jinsi anavyompenda na kumwuliza nini anamuoa mdogo wake badala yake?

Fimbo anamtimua na kumwambia moyo wake uko kwa mdogo wake na si yeye.

Mpumbavu naye amekufa na kuoza kwa Siwajibu, anamwambia ya moyoni, lakini binti huyo anamjibu kuwa yeye anampenda ndugu yake Fimbo na si yeye.

Siku ya harusi inafika, lakini kabla ndoa haijafungwa biharusi anaanguka na alivyozindua amepata wendawazimu.

Ni kichaa, kilichofuata sherehe ikavunjika, kijiji kikachafuka na aliyetuhumiwa kumroga ni kungwi wake, mke wa Muhogo Mchungu.

Mpumbavu naye anaanika kuwa aliyemroga Sikujua ni dada yake Siwajibu kwa sababu hakutaka aolewe na Fimbo kwa kuwa naye alikuwa akimpenda.

Mama kwa hasira anamfukuza Siwajibu nyumbani.

Mwisho wa siku ikabainika kuwa Sikujua alipatwa na uchizi kwa sababu mama yake alikwenda kwa mganga kwa ajili ya kuchukua dawa ya kumfunga ili asidhuriwe na watu wabaya wakati akiwa ndani. Mwali anafungwa dawa 'asirogwe' hadi siku ya kuolewa. Kwa bahati mbaya kwa mujibu wa mganga mhusika badala ya kumpa dawa ya kumfunga alimpa ya dawa tofauti ya mteja mwingine. Hivyo akaharibu.

**Simu 0716 350534.**
**afungamwango@gmail.com**



# RASMI J LO KIZIMBANI

SASA ni rasmi Jennifer Lopez, ameingia kwenye mgogoro na sheria kwa madai ya wizi wa wazo la shoo ya staili ya kucheza kutoka kwa msanii mwenzake.

Anadaiwa kuiba wazo hilo kwa dogo mmoja anayejilikana kwa jina la Alvin Gray-El aliyeliwasilisha kwa mbobezi wa unenguaji huko Marekani.

J Lo anayetamba kwa kukwaa umaarufu baada ya kuachilia vibao vikali vilivyoteka anga na kumpa umaarufu mkubwa mojawapo kikiwa ni my love doesn't cost a thing, sasa yuko matatani.

Dogo huyo anamtikisa mama huyo mwenye JLo akidai alimwibia mitindo ya kunengua anayoionyesha katika shoo ya World of my Dance 'WoD' na kudai mwana dada huyo mkali wa muziki huko Marekani amlipe Sh trilioni 1.4 ambazo ni Dola milioni 6.5.

Alvin alidai aliwasilisha wazo lake la uchezaji kwa mtaalamu wa minenguo Debbie mwaka 2009. Na kwamba onyesho lake lilikuwa lipewe jina la "Let's Start the Dance."

Alvin, anasema hata hivyo hakuwahi tena kupata taarifa zozote kutoka kwa Debbie, ambaye pia anamshitaki.

Anasema hata baada ya kusajili wazo lake na Shirika la Hati Miliki la Marekani , miaka saba baadaye aliambiwa kuwa kuna wazo kama hilo ambalo limesajiliwa tena ni mali ya J Lo na Televisheni ya NBC.

Alvin analalamika kuwa aliandika barua kwa viongozi wa NBC kuwaambia kuwa shoo inayonyeshwa na J Lo ni wazo lake alililowasilisha kwa Debbie. Lakini hakujibiwa.

Hata hivyo Alvin hajaweza kuelezea jinsia wazo lake lilivyochomoka kutoka kwa Debbie hadi kwa Jennifer, lakini kubwa anadaiwa Dola milioni 6.5.

Jennifer Lopez alizaliwa mwaka 1969 huko Bronx, NewYork na baba Guadalupe na David, anatisha kwenye anga za burudani kuanzia mwaka 1997 tena ni mahiri na mkali wa kuimba, kucheza na kuigiza.

# Britney Spears kawa kichaa?

BRITNEY Spears, amelazwa katika hospitali ya wagonjwa wa afya ya akili kwa kile kinachoelezwa kuwa ni kuchanganyikiwa kutokana na maradhi yanayomsumbua baba yake.

Vyanzo vilivyokaribu na nguli huyo anayeimba, kuandika mashairi na kucheza muziki na anayetisha kwa kuwa na mvuto wa kipekee huko Marekani, vinasema anaumia na kutatizika akili kunakotokana na ugonjwa wa baba yake.

Baba yake Jamie Spears, amefanyiwa operesheni mbili kutibu matatizo ya utumbo mpana.

Baba huyo alifanyiwa operesheni karibuni lakini kiafya anazidi kuwa dhoofu.

Jamie alianza kuumwa mwaka jana baada ya kupata tatizo la kuchanika mara kwa kwa utumbo mpana.

Britney aliweka pembeni nyumba yake ya Vegas ili kukaa na kumhudumia baba yake na kwamba ana wakati mgumu na shughuli nzito.





## Kardashian na kachanga

KIM Kardashian West na mume wake Kanye West wanatarajia wakati wowote kupata mtoto wa nne ambaye kwa mujibu wa maelezo yao ni mvulana. Jina analotarajiwa kupewa linaanza kusakwa kwa udi na uvumba.

Kim na dada zake Kourtney na Khloe walitinga kwenye kipindi cha runinga cha Jimmy Kimmel Live, kuzungumzia ujio wa dogo huyo..

"Nafikiria kumwita Rob, jina la kakangu " anasema lakini pia anaongeza naona jina la Robert, linafaa na kaka yangu amelikubali.

## Kasiri la 50 Cent lauzwa

RAPA 50 Cent wa Marekani, hatimaye ameuza kasiri lake lililoko Farmington, jijini Connecticut.

Jumba hilo lina uwanja wa eneo la heka 50,000, vyumba 19 vitanda 25, mabafu 25, uwanja wa mpira wa kikapu, bafu la chemchemu ya maji moto, sebule ya kukaa kwa raha watu 40, vyumba vyenye michezo mbalimbali, uwanja wa mazoezi ya viungo, studio ya kurekodi muziki, ukumbi wa sinema na klabu ya usiku.

Hivi karibuni aliliuza jumba hilo la kifahari kwa bei pungufu ya Dola milioni 2.9 ikiwa ni chini ya bei ya awali aliyokuwa anaitaka, alilenga milioni 18.5, mauzo hayo ni pungufu ya dola million 1.0 kiasi alicholipa mwaka 2003 aliponunua jumba hilo.





## Amber- Rose ni mjamzito

'ALEXANDER 'AE' Edwards pamoja na mimi tuna furaha ya ajabu kuwatangazia kuwa tunangojea kwa shangwe mtoto wetu wa kiume. Yuko njiani anakuja ni baby boy... PS Sebastian ana kila sababu ya kushangilia kuwa sasa anakuwa kaka mkubwa.

Anaandika Amber Rose kueleza kuwa ni mjamzito. Amber Rose ambaye ni mpambaji video maarufu Marekani aliyepitia misukosuko mingi katika muda mfupi anaongeza mtoto wa pili.

## Omotola afanya yake

MCHEZA sinema wa Nigeria –Nollywood, Omotola Jalade-Ekeinde, amechapisha kwenye ukurasa wake wa Instagram taarifa zenye hisia kali zinazoonyesha namna binti yake wa kwanza alivyonusurika kifo kutokana na tatizo la ubongo lililotokana na kiharusi.

Binti wa kwanza wa Omotola anayeitwa Princess, hivi karibuni alitimiza miaka 22 na katika kusherehekea siku yake ya kuzaliwa , baba yake Omotola alimpa zawadi ya gari la kisasa.

Katika hafla hiyo Omotola alimvalisha taji la kumtangaza kuwa ni mwanamke anayeheshimika na anayevutia wengi.

.... Kalikuwa kadogo kakapata homa kali haikushuka ghafla akapata kiharusi tulilia kama wenda wazimu....



**SAFU**



## Mionzi ya Sheria

**Na John Juma**
**0716217615**

# Ujue ni faini au jela ukikaidi kutunza mtoto

WAKO watu wanaolichukulia suala la kutoa mahitaji kwa mtoto kama suala au jambo la kawaida. Wakidhani ni la mama mzazi na baba mzazi.

Wanajidanganya eti ni suala la kuzungumza na likaisha kwa maelewano yoyote yale. Kama bado una mtazamo wa aina hii unahitaji kubadilika.

Kama hutabadilisha fikra subiri siku moja mkono wa sheria ya mtoto ukubadilishe. Suala la mahitaji ya mtoto ni jambo ambalo lina misingi kisheria na liko kwenye viwango vya kujadiliwa na kuadhibiwa si kukubaliana kama watu wanavyodhani. Si kitu ambacho unaachiwa uamue unavyotaka kwakuwa wewe ndiye mwenye mtoto.

Moja ya msingi wa hoja hii ni kwamba hakuna kusema sina hela za kugharamia mahitaji.

Huwezi kutakiwa kutoa mahitaji ya mtoto ukasema huna. Kama si mgonjwa asiyejiweza ama vinginevyo, jambo la kukosa fedha au mahitaji ya mtoto halikubaliki.

Pili, hata ukitakiwa kutoa ni wajibu kutoa kile ambacho kwa akili ya kawaida kitamwezesha mtoto kuishi kama binadamu wengine siyo kutoa Sh 200. Mzazi hatatoa chini ya kiwango cha ubinadamu.

Ndio maana suala hili si la kuisha kwa namna yoyote tu ambayo mhusika anafikiria. Anadhani anaweza kufanya anavyopenda.

Matunzo ya mtoto si jambo la kupelekana Idara ya Ustawi wa Jamii au pengine mahakamani , serikali za mitaa au kwa wazazi na kupewa amri ya kulipa fedha basi. Sivyo mchakato wa kisheria.

Ni kweli Idara ya Ustawi wa Jamii utapelekwa na mahakamani utafikishwa ila ni kuwa maamuzi hayaishi kwa wepesi.

Zipo adhabu za kisheria ambazo waweza kupata kwa kutotoa mahitaji ya mtoto.

Mwongozo wa Sheria kuhusu adhabu, unapatikana katika kifungu cha 51 (b) cha Sheria ya Mtoto Tanzania, 2009, kinatoa adhabu kwa yule anayeshindwa kutoa mahitaji kwa ajili ya mtoto kuishi na kwa ajili ya maendeleo yake. Kifungu hiki kinatofautisha kati ya mahitaji kwa ajili ya mtoto kuishi (necessities for survival) na mahitaji kwa ajili ya maendeleo ya mtoto (necessities for development).

Mahitaji kwa ajili ya mtoto kuishi ni kama chakula, wakati mahitaji kwa ajili ya maendeleo zaidi ni elimu. Ili uwe salama yote mawili ni lazima yapatikane hii ni kutokana na kifungu hiki.

Aidha, kifungu kimetoa adhabu za aina tatu kwa mtu atakayeshindwa kutoa mahitaji hayo kwa mtoto. Kwanza, ni adhabu ya faini, kinaainisha faini ya fedha taslimu isiyopungua Sh. 500,000 na isiyozidi 5,000,000. Kwahiyo humo katikati unaweza kuambiwa kulipa milioni 3 ama nne pengine mbili au 700,000, pengine 900,000 kutegemeana na maamuzi.

Kumbuka hii ni faini na si matunzo unayotakiwa kutoa. Ni penalti. Ni adhabu ya ukorofi.

Kwa maana ukilipa hii bado itatolewa amri nyingine ya kutoa mahitaji kama inavyostahili.

Pili, ni kifungo jela kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka mitatu. Humo katikati waweza kufungwa miezi saba, nane, tisa, 10 au mwaka mmoja , miwili na tatu.

Kumbuka kufungwa si mbadala wa kutoa mahitaji ya mtoto. Utafungwa na ukitoka huko jukumu la kutoa mahitaji linabaki palepale. Isitoshe, kifungu cha 166 cha Kanuni ya Adhabu Tanzania, Sura namba 16 pia inaeleza, tendo la kutotoa mahitaji ya mtoto kama ni kosa la jinai.

Tatu, ni adhabu ya vyote viwili yaani kifungo pamoja na faini. Jela utakwenda na faini utatoa. Hii nayo si mbadala wa mahitaji ya mtoto. Utatumikia adhabu zote na si sahihi , kuendelea, kulichukulia mzaha jambo hili kwani linaweza kuathiri mustakabali wako mzima wa maisha. Hii ni kwa njia moja au nyingine, hivyo acheni kupuuza kutoa mahitaji ya watoto.

Ni lazima kuwajibika na kujiepusha na kuzaa watoto usioweza kuwalea. Tafakari acha mwenendo mbaya.



## Kalamu ya Mwalimu

**Reubeni Lumbagala**

# Kamati za mitihani ni muhimili elimu bora

KATIKA kuhakikisha taifa linapata wasomi walioandaliwa kikamilifu wenye umahiri kwenye taaluma walizosomea, ni lazima uvujaji wa mitihani udhibitiwe kikamilifu.

Njia mojawapo ya kupima uelewa wa watahiniwa ni lazima wapimwe kwa mitihani kuanzia ya nadharia na ya vitendo. Hivyo basi, kutokana na unyeti wa nafasi ya mitihani katika kupima na kupata watahiniwa bora, ni vyema suala la mitihani likasimamiwa ipasavyo ili kuziba mianya nyote ya kuiba mitihani.

Mwezi uliopita, (Machi 26, 2019), Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alifanya kikao maalum na Maofisa Elimu Mikoa na Wilaya jijini Dodoma.

Kikao hicho kilikuwa ni maalum kwa ajili ya ufunguzi wa mkutano mkuu wa sita wa Umoja wa Maofisa Elimu Mikoa na Wilaya (Redeoa).

Mkutano huo ulichagizwa na kauli mbiu isemayo "elimu bora itatufikisha katika uchumi wa kati ifikapo 2025".

Katika mkutano huo Waziri Mkuu Majaliwa alizionya kamati za mitihani za mikoa na wilaya ambazo baadhi yao hushiriki katika udanganyifu wa kuvujisha mitihani kwa watahiniwa kuacha.

Hali hiyo inavunja heshima ya nchi kitaifa na kimataifa. Waziri Mkuu anasisitiza kwa kamati hizo za mitihani za mikoa na wilaya kuendelee kusimamia sheria, kanuni na taratibu bila ya woga wala upendeleo. Aidha, zisiyumbishwe na kuongeza kuwa hatua za kinidhamu za kiutumishi kwa mujibu wa sheria zitachukuliwa kwa wahusika.

Lakini, ni muhimu hatua za kinidhamu ziendelee kuchukuliwa dhidi ya wote wanaobainika kukiuka sheria, taratibu na miongozo inayotolewa kusimamia masuala nyeti kama mitihani.

Baraza la Mitihani la Taifa (Necta) ndilo lenye dhamana ya kuandaa mitihani ya taifa na hushirikiana na kamati hizo za mitihani za mikoa na wilaya kuhakikisha kuwa watahiniwa wanafanya mitihani kwa utaratibu wa kisheria na kiusalama kote nchini.

Uvujaji wa mitihani unaweza kutokea kipindi cha utungwaji, usambazaji na hata ndani ya vyumba vya mitihani kupitia walimu na wasimamizi.

Baraza hilo la mitihani kama wadau na wahusika wakuu wa utungaji wa mitihani, wanapaswa kutimiza wajibu wao katika kuhakikisha wote wanaoshiriki katika kazi hiyo wanafanyakazi kwa maadili na kutunza siri ili kulinda heshima ya mitihani.

Ni lazima uadilifu, uaminifu na uzalendo utangulizwe kwa wote wanaoshiriki kutunga mitihani ambayo itakuja kutumiwa kuwapima na kuwachuja watahiniwa ili kupata wahitimu bora wanaohitajika sana katika maendeleo ya nchi.

Watanzania wanaendelea kuamini kuwa watunzi wa mitihani watafanya kazi hiyo vizuri na kwa usiri mkubwa, hivyo waendelee kudumisha sifa hiyo njema waliyojijengea.

Baada ya Baraza la Mitihani la Taifa kumaliza kazi yake ya kutunga mitihani, kazi ya usambazaji wa mitihani hiyo kwa ngazi za mikoa na wilaya kufanyika na hapa ndipo kamati za mitihani za mikoa na wilaya hushika usukani.

Kamati hizo za mitihani baada ya kupokea mitihani hiyo, hushiriki katika kuitunza hadi siku ya mtihani itakapowadia na kuanza kuisambaza katika shule mbalimbali za msingi na sekondari ili wanafunzi waanze kutahiniwa.

Rai iliyotolewa na Waziri Mkuu Majaliwa kwa kamati za mitihani za mikoa na wilaya inapaswa kufanyiwa kazi ili kuhakikisha usiri uliotawala katika utungaji wa mitihani unaendelea kudumishwa kuanzia usambazaji wake, ufanyaji , usimamizi hadi inaposambazwa kwenye vituo mbalimbali kwa ajili ya kusahihisha.

Kazi inayofanywa na walimu wateule wa jukumu hilo maalum.

Kamati za mitihani pia huhusika kuchagua walimu wasimamizi wa mitihani hiyo. Kwa kuwa wasimamizi nao ni wadau muhimu katika kuzuia uvujaji wa mitihani ziwasisitize wanaosimamia kuwa na maadili na uadilifu.

Kamati ziwalishe viapo vya kazi hiyo maalum ili kuiepushia fedheha ya kuvuja kwa mitihani na hatimaye kusababisha kupata wahitimu vihiyo.

Kauli mbiu ya mkutano huo wa maofisa elimu ilisisitiza kuwa elimu bora itasaidia kufikia uchumi wa kati. Je, taifa linaweza kupata wahitimu bora kama kadhia ya kuvuja kwa mitihani itaendelea?

Jibu ni hapana. Hivyo basi, ni vyema kamati za mitihani kwa kushirikiana na walimu zikazingatia dhamana kubwa waliyopewa katika usimamizi wa elimu yetu kwa kuhakikisha taifa linapata wahitimu bora kwa kumaliza tatizo la kuvuja kwa mitihani.

Hakuna faida ambayo nchi inapata kwa kuvujisha mitihani zaidi sana ni fedheha kwa taifa kwani linakosa rasilimaliwatu wenye weledi wa kutosha katika taaluma walizozisomea.

Ndiyo maana walimu wanasisitiza kuwa wanafunzi wafundishwe kikamilifu na kwa weledi. Pia, wapewe mazoezi, majaribio na mitihani ya kutosha ili mtihani wa mwisho wafanye kwa uwezo wao na wanaostahili kufaulu ndiyo wafaulu ili kujenga taifa lenye elimu halisi.

Kama taifa ifike wakati kadhia ya uvujaji wa mitihani ili heshima ya nchi izidi kudumu kitaifa na kimataifa. Tafakari.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilayani Kongwa, Jijini Dodoma.

**Maoni: (+255) 764 666349.**



Na Elizabeth Zaya

NYUMBA YANGU

# Nyumba ni biryani yakhe...

ILI nyumba iwe na furaha na watu wajisikie kuwa wapo nyumbani, msosi ni suala la kupewa kipaumbele, tena si kuchemsha na kuupakua bali kuwa na ujuzi wa mapishi.

Licha ya kwamba tumekuwa tukizungumzia mambo mengi yanayohusu makazi kama usafi, mpangilio nyumbani kwa kuangalia ndani na nje, kutunza bustani, kuchagua eneo la kupanga na aina mbalimbali za vitanda, yote hayo si utimilifu kama hakuna ujuzi wa kuandaa mahanjumati.

Mapishi ni muhimu bila kujali ukubwa wa familia ili kuongeza chachu ya upendo, furaha na Amani ya nyumba. Pale ambako watoto hawajashiba siku zote ni shida hakuna uchangamfu bali ni hasira na ugomvi.

Mapishi ni lazima tena kuleta mahanjumati kitofauti, si kila leo kula ugali na mchicha au ubwabwa na maharage, jaribu kuandaa pilau, chapatti na leo muhsusi biriani, chakula ambacho asili yake ni India.

Kama ambavyo dunia kwa sasa huitwa 'kijiji' kutokana na ukuaji wa kasi wa teknolojia ya habari na mawasiliano, kila mmoja anaweza kujifunza kutoka kwa wengine na hata Watanzania wanapata pia elimu kupitia mitandao. Hata mapishi ya Kihindi pia ni vyema kujifunza.

Mohamed Mchowera, au Mudi Mabiriani mkazi wa Sinza Mori, jijini Dar es Salaam, ni bingwa wa kupika msosi huo, anasema 'birii' hutumika sana katika familia yake na amewekeza kwenye kuandaa chakula hicho kitaalamu na kuuzia wateja. Mchowera, anaeleza kuwa chakula hicho hutumika mahali popote pia nyumbani ndipo mahali sahihi zaidi kwa ajili ya watu kujichana na kujifurahisha.

"Maandalizi ya chakula hiki yanahitaji saa nyingi, kwa sababu mtu ambaye anakula biriani kesho mchana, maandalizi yake lazima yaanze leo, kwa hiyo lazima kuwapo na muda wa kutosha wa kuweka vikombwezo vyote na vikorokoro muhimu,"anasema Mchowera na kuongeza:

"Si chakula kigumu kupika isipokuwa namna ya kuandaa viungo vyake mpaka vikolee kikamilifu hasa vya kuweka katika 'sosi' au rojorojo ndivyo vinavyohitaji umakini mkubwa. Ila nikuhakikishie kwamba kuna haja ya familia kupendelea kutumia chakula hiki katika hata kama ni mara moja kwa wiki ni muhimu, inapendeza."

Anasema kwa wanaofahamu asili ya chakula cha biriani ni kuwaleta watu pamoja ili kudumisha umoja na upendo nyumbani.

Mchowera anasema anatengeneza chakula hicho kila mwisho wa wiki huko Sinza Mori na sasa amekubalika na amekuwa akipata 'oda maalum' za kupeleka kwenye nyumba za wateja.

"Mimi naandaa biryani kila mwisho wa wiki. Inapofika Ijumaa jioni watu wengi wanapenda kula chakula hiki wakiwa nyumbani na familia zao na hata watoto wakisikia kinapikwa hawachezi mbali na utawaona kabisa kwamba wanataka kupata kitu roho inapenda,"anatamba Mchowera na kuongeza:

"Hiki chakula kama nilivyosema hata kama nyumbani kulikuwa kumekosekana upendo, Amani na furaha kikipikwa furaha tele. Biriani ikiandaliwa utaona watu wanapatana. Ni lazima mpatane tu."

Anasema kwa asili kinaliwa juu ya mkeka mmoja na kinapakuliwa katika sinia moja pana kwa sababu wanasema ndiyo kinavyozidi kunoga zaidi lakini haizuiliwi kila mmoja kula sahani yake.

Anasema harufu ya chakula hicho kinapokuwa jikoni inaifanya nyumba iwe tofauti.

"Kwanza ukisikia harufu kinapoandaliwa ndani ya nyumba utatamani uendelee kuwepo humo. Yaani nyumba inakuwa na harufu ya kuongeza hamu ya kula na kutamani mlo unaondaliwa kama ni mgeni umepita njia, utaitamani ukaribishwe,"anasema Mchowera.

Kama nyumbani hakuna mtu anayeweza kupika biriani, upo umuhimu wa kujifunza, anashauri mpishi huyo na kuongeza kuwa usafi wa vyombo vinavyotumika kwa ajili ya maandalizi ya chakula hicho lazima uwe wa hali ya juu na kutunzwa katika mazingira safi muda wote.

Pia anashauri kwa nyumbani kwenye mazingira ya eneo linalotumika kuandaa chakula hicho pamoja na panapopikiwa lazima pawe safi kwa kiwango cha juu.



Mohamed Mchowera maarufu kama Mudi Mabiriani akiandaa msosi ofisini kwake Sinza Mori, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOHN BADI**



MAKALA

# Malezi ya mapacha wanne waliozaliwa kwa mkupuo

## ■Watimiza miaka mitatu, kuanza chekechea

Na Beatrice Moses

KUNA msemo wa Waswahili kuwa kwa kila jambo ni kumshukuru Mungu. Ndiye anayesimamia kila alifanyalo mtu liwe gumu au jepesi ndiye anayefungua milango na kumvusha mwanadamu popote.

Katika jukumu la kulea na kukuza mtoto kwa kimo na kiroho hadi awe mtu mzima anayejitegemea, wazazi wanamhitaji mno Mungu, lakini pia wanashukuru kushikwa mkono na marafiki pamoja na jamaa zao.

Ndivyo wazazi wa watoto wanne waliozaliwa kwa mkupuo Aprili 4 mwaka 2016 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), wanavyomshuru Mungu na marafiki waliowasaidia kuanza na kuendeleza safari ya kuwalewa watoto wao.

Licha ya kwamba sasa wanakuna vichwa, hasa kipindi hiki wanapotimiza miaka mitatu, ambako kunawasogeza kwenye hatua nyingine wana imani kuwa Mungu pamoja na marafiki watatembea pamoja nao katika safari yao.

Watoto hawa mapacha wanne ni Ngasa (wa kiume) na wenzake watatu wa kike; Debora, Dorcas na Delicia Mafuruka, wanatakiwa kuanza safari yao ya elimu wakati wowote kuanzia sasa.

Akizungumza na gazeti hili, mama wa watoto hao, Sara Dimoso anasema wanatafakari gharama za kuwasomesha watoto hao, ikiwamo shule watakayosoma kuanzia sasa, kwa kuwa umri walionao unawaruhusu kujiunga na shule ya awali.

"Tunapenda wasome kwenye shule yenye mazingira mazuri na inayozingatia maadili, tunaamini hiyo itawasaidia kuwa na tabia njema kwa sababu wanashahibiana hivyo huigana tabia, "anasema. Sara.

Anabainisha kuwa wanamshukuru Mungu licha ya changamoto za malezi na gharama kubwa za maisha, wanaendelea vyema sasa wanaweza kujieleza kiasi cha kueleweka, hatua ambayo imetoa unafuu katika kuwahudumia.

Pia, kule kuugua magonjwa ya kuambukizana kumepungua kwa kiasi kikubwa tofauti na ilivyokuwa awali, ambapo akiungua mmoja basi wengine nao wanaugua hivyo wanalazimika kuwapeleka wote hospitali, anaeleza mama huyo.

"Wanaendelea vizuri Ngasa kwa sasa amefikisha kilo 18.3 anapenda kula hivyo chakula kinapowekwa mbele yao huanza kula mwenyewe tofauti na wenzake ambao hutegemea kulishwa," anasema Sara na kuongeza:

"Mtoto wa pili, Deborah kwa sasa ana kilo 13.5 hapendi wageni, akiwaona huwakwepa hataki pia kuchangamana nao, ingawa yupo makini na anapenda kucheza mwenyewe. Mwanangu wa tatu, Delicia kwa sasa ana uzito wa kilo 12.6 anapenda watu, anapendelea kucheza muziki na kuimbaimba."



Sara Dimoso na watoto wake : **PICHA ZOTE : BEATRICE MOSES**



Sara anasema Dorcas ndiye mdogo kuliko wote ana uzito wa kilo 12.2 ni mwepesi wa kuelewa, anaelewa vitu haraka, pamoja na kuigiza wanavyofanya wenzake.

**CHANGAMOTO**

Sara anataja miongoni mwa changamoto alizokutana nazo kuwa ni pamoja na kulazimika kubadili wasaidizi wa kazi za nyumbani mara kwa mara.

"Tumeshabadili kama watano kutokana na sababu tofauti wapo waliohitaji kulipwa Sh100, 000 wakati kipato chetu hatuwezi kumudu gharama hiyo. Gharama kubwa ya kuwahudumia hawa watoto ikiwamo maziwa ni jambo jingine ningependa kulizungumzia. Wanakunywa lita 15 kwa wiki," anasema Sara.

Sara anasema pia imekuwa vigumu kuwatembelea ndugu na jamaa, au kuhudhuria kwenye sherehe kwa sababu watoto wake wanahitaji kuhudumiwa kwa namna ya kipekee.

Anasema kama ilivyo kwa mapacha watoto hao wanapenda kufanya vitu kwa kuigana, hivyo hata mavazi kwa asilimia kubwa wanalazimika kuwanunulia yanayofanana.

**NAWASHUKURU WANAOTUSAIDIA**

Abednego Mafuruka baba wa watoto hao anafanya kazi katika Mgodi wa Geita Gold Mine (GGM) mkoani Geita, anaeleza kuwa anafarijika kuona watoto wake wakiendelea vyema kiafya.

Anasema japo muda mwingi anaishi mbali nao lakini amekuwa akijitahidi kuwasiliana na familia yake, ikiwamo kuhimiza umakini katika malezi yao kwa ujumla.

Mafuruka anasema wanajumla ya watoto sita, kwani kabla ya kuzaliwa wanne hao kuna dada zao wawili, hivyo Mungu aliwabariki na kuiongeza familia hiyo kwa kiwango hicho.

"Katika mawazo yetu ya kibinadamu hatukutarajia kupata baraka hii ni Mungu mwenyewe ametubariki, tunashukuru hata jinsi anavyowainua watu na taasisi kuona jukumu kubwa tulilo nalo hivyo kujitolea kutusaidia kiasi," anasema.

Anataja taasisi zilizojitokeza kusaidia wanandoa hao kuhudumia watoto hao walipozaliwa kuwa ni pamoja na Benki ya NMB, Kanisa la TAG Kijitonyama na Kanisa la KKKT Korogwe.

Pia aliyekuwa Mkurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Julieth Kairuki, ambapo anawashukuru akiwasihi waendelee kuwakumbuka hata katika kipindi hiki wanapotarajiwa kuanzishwa shule. "Ndoto yetu ni kuwaona wanakuwa na afya njema, wanasoma shule yenye mazingira rafiki, kwa kuwa wapo wanne ni gharama kubwa kulipa ada kwa mkupuo kama watapata fursa ya kusoma shule za binafsi zilizopo karibu na nyumbani kwao," anasema.

# Wadau usalama barabarani wawaibua wamachinga

Na Mary Geofrey



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola na Naibu Waziri, Hamad Masauni, wakipewa maelezo namna kitengo cha usalama barabarani kinavyotekeleza majukumu yake katika kongamano lililofanyika wiki iliyopita jijini Dar es Salaam. **PICHA: MARY GEOFFREY.**

WIKI ya Nenda kwa Usalama Barabarani ambayo hufanyika kila mwaka kwenye mikoa mbalimbali nchini, kwa lengo la kutoa elimu kwa watumiaji wa barabara, wakiwamo madereva, wasafiri na watembea kwa miguu, suala la kutafuta mikakati ya kupunguza ajali ndicho kipaumbele.

Ili kutimiza azma hiyo mwaka huu Jeshi la Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani, limeandaa kongamano lililowakutanisha wadau mbalimbali kuchambua na kuweka mikakati ya kuimarisha usalama.

Kongamano hilo liliwaleta pamoja Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni na Katibu wa Baraza hilo, ambaye pia ni Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Muslim.

Kadhalika liliwakutanisha Wakuu wa Polisi mikoa yote nchini, Makamanda wastaafu wa Kikosi cha Usalama barabarani ambao pia ni wajumbe wa baraza na wamiliki wa mabasi na asasi za kiraia za kutetea abiria na watumiaji wa barabara.

Lengo kuu lilikuwa ni kupokea taarifa ya hali ya usalama barabarani nchini, changamoto na kujadili namna ya kukabiliana nazo hasa katika kuhakikisha wanapunguza ajali hizo nchini. Akifungua kongamano hilo, Waziri, Kangi Lugola, anasema kusanyiko hilo linawapa fursa wadau kujua wanakwama wapi katika kukabiliana na changamoto zinazopelekea ajali za barabarani ambazo hupoteza maisha ya watu wengi.

Lugola anasema yaliyo kwenye uwezo wake anayatekeleza ikiwamo kuwachukulia hatua za kisheria madereva wanaovunja sheria, kusimamia sheria na kuwachukulia hatua askari wanaokiuka maadili ya kazi.

Anaeleza pia kwa sasa changamoto kubwa iliyopo katika jeshi hilo ni polisi wasio waadilifu wanajihusisha na vitendo vya rushwa vinavyosababisha kupoteza haki za wanyonge na kuchangia kuendelea kwa vitendo vya uvunjifu wa sheria zilizowekwa.

"Hivyo nawakumbusha tena, maofisa na askari wasiotaka kubadilika na kuacha rushwa siku zao zinahesabika kwani taarifa ya kamati niliyounda hivi karibuni ya kuchunguza vitendo hivyo katika kikosi cha usalama barabarani tayari iko mezani kwangu," anasema Lugola.

Anawataka polisi kusimamia sheria na kujiepusha na vitendo vya rushwa ili kuokoa maisha ya watu wasio na hatia ambao hufariki dunia huku wengine hupata ulemavu wa kudumu kutokana na ajali za barabarani.

### HALI YA AJALI

Waziri Lugola anasema kwa mujibu wa takwimu, kuanzia Januari hadi Desemba mwaka 2017, ajali 5,574 zilitokea nchini ambazo zilisababisha vifo 2,581 na majeruhi 5,489.

Anasema katika kipindi kama hicho mwaka 2018 kulitokea ajali 3,732 ambazo zilisababisha vifo 1,788 na majeruhi 3,746 na kufanya tofauti ya ajali kuwa 1,842, vifo 793 na majeruhi 1,743.

"Hivyo natumia fursa hii kulipongeza Baraza, Jeshi la Polisi kikosi cha Usalama Barabarani, madereva, wadau wa usalama barabarani na wananchi kwa ujumla kwa kufanikisha kupunguza ajali kwa asilimia 31 na vifo kwa asilimia 31, mafanikio haya yanatokana na ushirikiano wa wadau wa usalama barabarani," anasema Lugola.

Vilevile Waziri Lugola, anasema asilimia 76 ya ajali za barabarani zinazotokea nchini hutokana na makosa ya kibinadamu ambapo kati ya hizo asilimia 40 ni uzembe wa madereva.

Anaeleza kuwa, kwa mwaka 2018 madereva 1,556 walisababisha ajali kwa uzembe, wakati 364 walisababisha ajali kwa mwendokasi, huku 61 wanatuhumiwa kwa ulevi na wengine 725 kwa walisababisha ajali kwa kuendesha pikipiki kizembe.

Pia watu 103 nao walisababisha ajali kwa kuendesha baiskeli kizembe na watembea kwa miguu 259 walisababisha ajali kwa uzembe wao. Lugola anasema ni wazi kwamba wasimamizi wa sheria wakizisimamia kikamilifu kwa kuendelea kutoa elimu kwa watumiaji wengine wa barabara ambao iwapo watabadili tabia uwezekano wa kupunguza ajali ni mkubwa.

Aidha, Waziri Lugola analitaka baraza hilo la Usalama Barabarani kusimamia ukaguzi wa magari ili kuhakikisha magari mabovu yanaondolewa barabarani.

"Baraza liweke msukumo wa uanzishwaji wa mfumo wa lazima wa ukaguzi wa magari ili uanze kutumika haraka nchini, " anasema.

Aidha analitaka likamilishe uundwaji wa kamati za usalama barabarani za mikoa na wilaya haraka ili kamati hizo zianze kazi kwa lengo la kwenda na mabadiliko yanayofanyika ndani ya baraza.

"Baraza liweke pia msukumo mkubwa katika mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya usalama barabarani yanayolenga kuleta mabadiliko ya muundo wa baraza kulifanya liwe baraza tendaji, kuwa na vyanzo vyake maalum vya mapato, liwe na waajiriwa wa kudumu wa kufanya kazi za kila siku za baraza, " anasema.

### WADAU

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Chama cha Madereva Tanzania, Majura Kafumu, ili kupunguza ajali za barabarani ni vyema madereva wakaandaliwa kwa mafunzo kabla ya kuruhusiwa kuendesha gari barabarani.

"Ni muhimu madereva wakapatiwa mafunzo lakini serikali ilione hili la barabara nyingi kutumiwa na wafanyabiashara wamachinga jambo ambalo linasababisha uwepo wa watu wengi barabarani," anasisitiza.

Wamachinga hupanga bidhaa barabarani, kwenye hifadhi ya barabara na wengine huuza bidhaa kama maji, matunda, vinywaji baridi ndani ya barabara na wakati mwingine kusababisha usumbufu na ajali.

Mratibu wa Kituo cha Usuluhishi (CRC) kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), Gladness Munuo, anasema kuwapo kwa sheria bora ya usalama barabarani kutapunguza ajali hizo na kama wadau na kuiomba serikali iharakishe kupeleka muswada wa mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani bungeni.

"Tunajua kuwa sheria hii ya mwaka 1973 inapaswa kufanyiwa mabadiliko hivyo tunataka kujua itafanyiwa kazi wakati gani?" alihoji Munuo.

Anasema pia ni muhimu Serikali ikawekeza kwa wadau kwa kutoa elimu kuhusiana na masuala ya usalama barabarani

Mwenyekiti wa Usalama barabarani kutoka Chama cha Madereva wa Malori Tanzania, Nditile Samson, anasema madereva wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kupata kipato kidogo kutoka kwa wajiri wao.

Anasema changamoto nyingine ya ajali ni maslahi hivyo wamekuwa wakiwabana sana madereva jambo ambalo linawafanya wakiwa safarini kufikiria vitu vingi hatimaye kusababisha ajali.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza hilo, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, anasema mwaka huu wameamua kufanya kongamano kama hilo, ili kupunguza gharama na kupata fedha za kununua magari ya askari.

Anasema kupitia fedha zinazopatikana kwa kuuza stika za magari na hizi ambazo zingetumika katika maandalizi ya maadhimisho ya wiki ya nenda kwa usalama, zitatumika kununua vitendea kazi vitakavyorahisisha utendaji kazi wa jeshi la polisi.

"Pia tunataka kuhakikisha fedha hizi za stika za usalama zinazobandikwa katika magari kila mkoa zinatumika pia kununua magari kwa ajili ya askari, " anasema Masauni.

Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Muslim, anasema oparesheni mbalimbali ambazo zimeanzishwa nchini kwa ajili ya kupunguza ajali zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza suala hilo.

Anasema wanaendelea na juhudi mbalimbali za kuhakikisha ajali hizo zinaendelea kupungua zaidi kwa kusimamia sheria na kuwachukua hatua wale wote wanaozivunja.

Anaeleza kuwa wanawachukulia hatua za kisheria ambao wanashindwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kukiuka maadili ya kazi ili kuhakikisha hakuna anayekwamisha juhudi hizo za serikali.

## HABARI KIMATAIFA

# Kibopa amtaliki mkewe kwa kitita cha dola bil. 35

**SEATTLE, Marekani**

BILIONEA anayemiliki mtandao wa Amazon, Jeff Bezos, na mkewe MacKenzie wamefikia makubaliano ya aina yake ya talaka yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 35.

Katika makubaliano ya talaka baina ya wawili hao, Bezos anapokea asilimia nne ya umiliki wa kampuni hiyo kubwa duniani.

Amazon iliasisiwa na Bezos, Seattle nchini Marekani mwaka 1994, mwaka mmoja baada ya wawili hao kuoana na wakati huo mkewe huyo alikuwa mmoja wa waajiriwa wa kwanza.

Baada ya kufikia mwafaka juu ya kuachana huko, wote walituma ujumbe kumhusu mwenzake baada ya tangazo hilo.

Hata hivyo, wawili hao hawakutoa taarifa ya ziada ya makubaliano ya kifedha yaliofikiwa.

Hisa za Amazon pekee zitamfanya mtalaka huyo wa Bezos kuwa mwanamke wa tatu tajiri huku Bezos mwenyewe akisalia kuwa tajiri mkubwa duniani, kwa mujibu wa jarida la Forbes.

Jeff Bezos, mwenye umri wa miaka 55 na MacKenzie mwenye miaka 48, walioana mwaka 1993 na wana watoto wanne.

Ujumbe wa Mackenzie katika Twitter ni wa kwanza na wa kipekee tangu kujiunga na mtandao wa kijamii mwezi huu. Katika ujumbe huo ameandika: "Nimeshukuru kukamilisha talaka yangu na Jeff kwa ushirikiano."

Bezos kwa upande wake ameandika: "Ninawashukuru rafiki zangu na familia yangu kwa kunipa moyo na kuonyesha upendo... zaidi MacKenzie."

Alikamilisha ujumbe huo kwa kuandika: "Ni msaidizi anayejituma na mwenye mapenzi, na wakati maisha yetu



Bezos na Mackenzie enzi za ndoa yao. **PICHA:MTANDAO.**

yanafunguka katika siku za usoni, nafahamu kwamba nitaendelea kujifunza kutoka kwake."

Kabla ya makubaliano hayo Bezos alimiliki asilimia 16.3 ya kampuni ya Amazon lakini ataendelea kushikilia asilimia 75 ya umiliki huo lakini Mackenzie amewasilisha haki zake zote za uamuzi kwa mtalaka wake.

Anakabidhi pia hisa zake alizokuwa anamiliki katika gazeti la Washington Post na kampuni ya safari za anga za juu ya Bezos, Blue Origin.

Amazon ni kampuni ya mtandao inayotumika pakubwa duniani katika biashara ya mauzo.

Mwaka jana, kampuni hiyo ilipata faida ya Dola za Kimarekeni bilioni 232.8 na imemsaidia Bezos na familia yake kukusanya utajiri wa dola bilioni 131b, kwa mujibu wa jarida la Forbes.

Januari 10, mwaka huu, iliripotiwa kuwa Bezos ambaye ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Amazon na mkewe MacKenzie wanatarajiwa kupeana talaka baada ya miaka 25 ya ndoa yao.

"Baada ya kipindi kirefu cha mapenzi na kujaribu kutengana, tumeamua kuachana na kuendelea na maisha yetu kama marafiki," wawili hao walisema kwenye taarifa yao ya pamoja.

Wakati wakitangaza kuachana huko, Amazon ilikuwa na thamani ya dola bilioni 797 baada ya kukua kwa asilimia 3.4 ikiipiku Microsoft ya Bill Gates yenye thamani ya dola bilioni 789.-

*BBC*

# Mahakama yafuta visa ya Bensouda

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imetanga kufuta Visa ya kuingia nchini humo ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita (ICC), Fatou Bensouda.

Uamuzi huo unadaiwa kuwa unatokana na uchunguzi wa Bensouda kuhusu uhalifu wa kivita uliodaiwa kufanywa na na vikosi vya Marekani na washirika wake nchini Afghanistan.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, hivi karibuni alionya kwamba nchi yake inaweza kuwakataa au kufutilia mbali Visa za maofisa wowote wa ICC wanaohusishwa na uchunguzi huo.

Hata hivyo, ofisi ya Bensouda ilisema kiongozi huyo wa mashtaka ataendelea na jukumu lake bila kuogopa au kupendelea upande wowote.

Pompeo alimwarifu Bensouda kuwa: "Iwapo unahusika na pendekezo la ICC la kuwachunguza wanajeshi wa Mare-



kani kuhusiana na hali ya Afghanistan, usidhani kwamba utaendelea kuwa na visa ya Marekani au kuingia nchini humu."

"Tumejiandaa kuchukua hatua zaidi ikiwamo vikwazo iwapo ICC haitabadilisha mwenendo wake", aliongezea Pompeo.

Ripoti ya mwaka 2016 kutoka ICC imesema kulikuwa na sababu muhimu kuamini kwamba jeshi la Marekani lilifanya utesaji katika kituo kimoja cha siri Afghanistan kinachoendeshwa na Shirika la Ujasusi la Marekani (CIA) na kwamba serikali ya Afghanistan na wapiganaji wa Taliban walitekeleza uhalifu wa kivita.

Marekani ambayo imekuwa ikikosoa ICC tangu ilipoanzishwa, ni miongoni mwa mataifa kadhaa yaliyojiunga na mahakama hiyo.

ICC ilianzishwa na Azimio la Umoja wa Mataifa mwaka 2002 na kuidhinishwa na mataifa 123, ikiwamo Uingereza lakini nchi kadhaa zikiwamo China, India na Russia zilikataa kujiunga.

Hata hivyo, kutokana na hukumu au uchunguzi unaofanywa na mahakama hiyo, baadhi ya mataifa ya Afrika yamekuwa wakielezea nia yao ya kujiondoa kwa madai ya upendeleo dhidi yao.-

*BBC*

# Bangi yadaiwa kuwa na kinyesi

**MADRID, Hispania**

BANGI inayouzwa katika mitaa ya Madrid imedaiwa kuwa ina viwango vya kinyesi ambavyo ni hatari kwa watumiaji, utafiti umeonyesha.

Kwa mujibu wa utafiti huo, chembe chembe za bakteria za E.coli na kuvu ya Aspergillus, zimegunduliwa na wakaguzi kutokana na uchunguzi uliofanyika kupitia sampuli 90.

Aidha, utafiti huo umeonyesha kuwa sampuli za 'Hashish' zilizofungwa kwenye mifuko ya plastiki ndizo zilizogunduliwa kuwa na viwango vikubwa zaidi na inaelezwa kuwa hiyo inatokana na namna zilivyoingizwa nchini humo.

Utafiti huo unaeleza zaidi kuwa asilimia 40 ya chembe chembe hizo zina harufu za kinyesi.

Wakati hayo yakibainishwa kununua, kuuza na kuingiza bangi ni marufuku nchini Uhispania kama vile ilivyo kinyume cha sheria kuivuta hadharani.

José Manuel Moreno Pérez, mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Complutense mjini Madrid, alikusanya 'hashish' inayofahamika kwa jina maarufu mitaani kama 'hash' au 'resin' kutoka kwa wauzaji maarufu mitaani mjini na katika viunga vyake kwa lengo la kubaini iwapo mihadarati hiyo inafaa kutumika na binadamu.

Kundi lake la watafiti baadaye lilizigawanya sampuli kwa umbo la namna zilivyoundwa kuona iwapo umbo moja lina uchafu huo ikilinganishwa na lingine. Utafiti huo umechapishwa katika jarida la Forensic Science International.

Utafiti huo umegundua kuwa baadhi ya sampuli hizo zina asilimia 93 ya viwango vya hatari vya bakteria ya E.coli na zingine zina kiwango cha asilimia 29.4 cha bakteria .

Pia asilimia 10 ya sampuli hiyo ya bangi iligunduliwa kuwa na kuvu hatari ya Aspergillus, inayoweza kusababisha matatizo makubwa kiafya na kwamba asilimia 88 ya sampuli zilizofanyiwa uchunguzi zimegunduliwa kuwa hazifai kutumiwa na binadamu.

*BBC.*

# HADITHI

AJALI kubwa iliyotikisa nchi inatokea eneo la Mikese mkoani Morogoro baada ya basi la abiria kuungua moto, kuua na abiria wengine kujeruhiwa.
Awali inachukuliwa poa kama ajali za kawaida. Lakini nyuma ya pazia, ni ajali iliyopangwa na muuaji , mwenye akili za kiwendawazimu, akibebwa na hisia za chuki, wivu na kisasi bila kujali madhara kwa watu wengine wasiohusika. Eddy Kamal, mpelelezi makini, anategua kitendawili hiki. Fuatilia kisa hiki....

# Kisanduku Cheusi-42

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MANENO aliyokuwa akiongea Eddy yaliwatisha mpaka mabausa watatu wa Mapunda. Tukio alilolifanya mle ndani hadi kuwaweka chini ya ulinzi na jinsi anavyosimulia alivyokuwa akilipeleleza jambo hilo, liliwafanya kuona wamejiingiza kwenye kazi nzito kuliko walivyodhani.

Jasho nao lilianza kuwatoka, ingawa walijitahidi kutoonyesha hofu ili kusubiri muda kwani wanaweza kuokolewa na wenzao huko nje iwapo watahisi kuwa wamo hatarini.

"Niporejea Dar, nilitaka kujua kuwa Banson Mapunda ni nani. Na wasaidizi wangu waliniletea zaidi ya watu 15 kwenye majina hayo, lakini lililonivutia ni jina la mtu huyo linaloonyesha kuwa ni Mkurugenzi Mtendaji na mmiliki wa Paradiso Hotel.

Ndiyo hoteli ambayo Careen na Hellen walikuwa wakifanyia kazi. Na Mapunda ndiye alikuwa mpenzi wake Careen. Na huyo huyo ndiye aliyeporwa mpenzi aliyeuawa katika mazingira ya kutatanisha.

Nilijua nikija kama mpelelezi nitachukua muda mrefu kupata ninachokitaka. Nikikukamata na kukuhoji tutasumbuana na huwezi kunipa ushahidi wa moja kwa moja. Nilichokifanya ni kujifanya mimi ndiye Mayambua na nikaja ofisi kwako. Nilijua kitu ambacho ukikutana na mtu kama huyo utamfanya. Kwa sababu tayari ulishamtisha.

Kwa bahati mbaya ulijifanya haupo ofisini, niliandika ujumbe na kumpa sekretari wako, nilijua akiupata tu na kuona jina la Mayambua ni lazima ashtuke na kuanza kunifuatilia. Na kweli ikawa hivyo, hadi wale watu wako waliponiteka. Nilihitaji kutekwa ili kujua haya niliyoyajua kwa wepesi na urahisi zaidi.

Ndiyo maana hata wewe mwenyewe ukaniambia kila kitu ulichokifanya juu ya mpango mzima wa kumuua Careen na watu wengine.

Hakuna ambacho umekifanya na hakijulikani kwa sasa bwana Mapunda utalipa unyama wote ulioufanya." Eddy alizidi kunguruma.

"Na kwa bahati mbaya sana kwako kushinda zote ulinisimulia siri zako zote na mipango yote uliyofanya mpaka ukatekeleza mauaji hayo.

Na ulifanya hivyo kwa sababu ulijua utaniua tu kwa sababu mimi ni raia dhaifu.

Ni Mayambua, aliyemchukua mpenzi wako, hivyo ulitaka auawe huku akijua ukweli wote. Ukweli mimi si Mayambua. Na vyote ulivyosema nilikufungulia awali ukasikia, nimerekodi na nitawapa polisi kama ushahidi kwa sababu ulisema mwenyewe kwa kinywa wako."

Tumbo lilianza kumcheza Mapunda. Kila alichokuwa akikisimulia Eddy kilikuwa ni sahihi. Kwa mara ya kwanza aliujutia mpango wake huo. Alijiambia kuwa haukuwa na maana kama angemuacha Carren aolewe na yeye kutafuta mchumba mwingine.

Kwa sasa ana mchumba mwingine aitwaye Getruda, anayetarajia kufunga naye ndoa hivi karibuni.

Lakini kutokana na vyote alivyofanya na mambo yote yanakaribia kuwekwa hadharani ili wananchi wa Tanzania wayasikie, na hiyo itamfanya ama atumikie kifungo cha maisha, au anyongwe.

Adhabu hiyo itamfanya kutomuoa Getruda, mwanamke ambaye ametokea kumpenda.

"Mapenzi ni kitu cha ajabu. Niliumia sana Careen kuchukuliwa na mwanaume mwingine. Nilidhani bila Careen siwezi kuishi, lakini leo najionea kuwa kumbe ningeweza kuvumilia na kumpata Getruda ambaye kwa muda mfupi amenisahaulisha machungu yote." Alijiambia Mapunda. Hata hivyo, yote hayo ni kama vile ile methali inayosema 'majuto mjukuu'.

Kila akiangalia mbele anakutana na kijana mkakamavu aliyekaa kwenye kiti mbele yake. Anayeonekana kuwa alipeleleza ishu nzima ya kulipua basi na kufanya uhalifu mwingine ambao awali alidhania kuwa ni Mayambua. Kijana aliyemnyang'anya mpenzi wake. Alijiona mpumbavu. Kosa dogo limesababisha mpango wote kabambe alioufanya kwa umakini na utaalam wa hali ya juu kuvurugika.

**Ni Mayambua, aliyemchukua mpenzi wako, hivyo ulitaka auawe huku akijua ukweli wote. Ukweli mimi si Mayambua. Na vyote ulivyosema nilikufungulia awali ukasikia, nimerekodi na nitawapa polisi kama ushahidi kwa sababu ulisema mwenyewe kwa kinywa wako."**


"Na kuhusu suala la kuondoka hapa jana usiku wala si filamu wala maigizo. Niliondoka kwenye jengo lenu kwa kutoboa juu na kuondoka. Nikaruka ukuta bila mtu yoyote kujua. Nikaenda hadi nyumbani kwangu. Nikaoga na kula. Nikachukua vifaa vyangu muhimu vitakavyonisaidia kwenye mapambano haya kwa sababu nilijua yatakuwepo, ikarejea kwa kutumia njia ile ile na hakuna hata nzi aliye ndani ya jengo hili aliyegundua hilo.Mtu pekee aliyejua hili, nilimmaliza."

Maneno hayo yalizidi kuwatisha Mapunda na walinzi wake watatu ambao walionekana kabisa wamenyong'onyea.

Inaonekana hawakupanga au kutegemea kukutana na mtu wa aina hii.

"Kwa taarifa yenu mimi kutoka humu ni mchezo mdogo tu kama wa kuwasha swichi ili taa iwake. Mimi ni askari mpelelezi mwenye uwezo wa kikomandoo, hivyo hamchezi na mtu wa wasiwasi."

Maneno yake waliyaamini, kwani kwa jinsi walivyoshuhudia mchezo ule waliochezewa wakati wanaingia ndani na jinsi alivyowaua Baunsa na mwenzake, waliona kabisa hawakuwa wanacheza na binadamu wa kawaida.




Kwa mbali Mapunda alihisi ganzi. Alianza kufikiria jinsi atakapokuwa akikabidhiwa mbele ya polisi na baadaye televisheni zote nchini pamoja na taarifa za habari za kwenye redio na mitandao ya jamii kumuonyesha yeye kuwa ni muuaji, aliyeua abiria wa basi la Bomoa Trans.

Alifikiria jinsi watu watakavyoshangaa kumuona Mkurugenzi Mtendaji na mmiliki wa hoteli kubwa nchini ya Paradise, ambaye alichukuliwa kuwa ni mtu mtiifu, mcha Mungu na mwenye kutoa misaada mbalimbali kwenye makundi ya jamii na serikali, lakini kumbe nyuma ya pazia ni mnyama zaidi ya chui.

Ni muuaji wa wauaji, aliyeua hata watu wasio na hatia kwa sababu ya mihemko yake ya kimapenzi. Alifikiria pia jinsi wananchi watakavyomlaani na kumuombea kila aina ya baya na kuitaka mahakama ifanye kazi yake haraka ili ahukumiwe.

Liwatafakari waliopoteza jamaa zao na basi la Bomoa , majeruhi na walemavu walioungzwa na bomu. Alizidi kujihurumia.

Alimfikiria vile vile mke wake mtarajiwa Getrude atakavyoangua kilio atakapoona tukio hilo kwenye runinga lakini baadaye, akitulia pia atamlaani na kuona ni mwanaume katili ambaye pia hata yeye akijichanganya anaweza kupata adhabu kama hiyo ya mwenzake au zaidi ya hiyo. Baada ya kufikiri vyote hivyo, Mapunda alionekana ni kama amepagawa. Aliona ni bora afe kuliko kuchukuliwa kama kuku na kuwekwa hadharani mbele ya Watanzania akiwa hai, huku akiwa na makosa mazito.

Ni bora tu kuhuma hizo zifike kwa Watanzania akiwa ameshakufa kwani hatopata aibu kama akiwa hai.

"Bora nife kuliko aibu hii." Aliwaza. "Lakini siwezi kufa peke yangu.Ni lazima nifanye kitu humu ndani ili kama kufa tufe wote." Aliwaza.

Wakati akiwaza hilo, kengele ya hatari ilianza kulia kwenye ubongo wa Eddy.

**Itaendelea Jumamosi**

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA, VIWANJA VINAUZWA CHANIKA** mita 100 kutoka stendi mpya ya Chanika. Umeme upo Bei kuanzia Mil.2. Kwa Mawasiliano: 0714 187555/ 0755 288879

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI UALIMU /** certificate au diploma /english/ mathematics /SST na science 0656490706/0655628640


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
05/04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya kesho tarehe 05/05/2019 kampuni ya **Kuku Nzima Ltd** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa Kutoka **TPC kuelekea KIA JUNCTION,** gari hilo lenye namba za usajili:T724 BDR
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 19.90**
   **Upana - mita 3.30.**
   **Kimo - mita 4.40**
3. Njia itakayotumika TPC ROAD hadi ARUSHA ROAD kupitia ARUSHA ROAD. gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115161102

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**RAPHAEL ROBART** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO **T134 DJH** ENGINE NO **16LO1962C** CHASSES S NO **SALLDHMF75A689730** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI **MON/RB 532/019.**

215161302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAGGIE PHILIP TEMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 111 AWK LAND ROVER.** CHASSIS NO; **LBCMHIAAF512439.** ENGINE **NO; 9029957.E.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/B.I/21/VOLIX/2009/2019.**

115161402


## CHETI KIMEPOTEA



**VICTORIA M. GEORGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0371-031** kilichotolewa na LOMBETA SECONDARY mwaka 1993. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **AR/RB/2511/2001.**

115160902

## KUPOTEA KWA VYETI



**Evaline S. Nassary** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo; Cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0223-0019** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2008 katika shule ya Sekondari ya wasichana Masama na cheti cha Ualimu chenye namba **E0517-0025** kilichotolewa na chuo cha Ualimu Kitangali mwaka 2011. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MOR/RB/145/2019**

115160702

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 06-04-2019 kampuni ya **DOW ELEF INTERNATIONAL TANZANIA LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea MTWARA** kupitia NANGURUKURU, gari hilo lenye namba za usajili:
   1. **T 505 DNJ/ T 863 DKM**
   2. **T 508 DNJ / T 858 CLY**
   3. **T 164 DNL / T 854 CLY**
   4. **T 181 DNL / T 865 DKM**
5. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 18.00**
   **Upana - mita 3.00**
   **Kimo - mita 5.00**

   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215162402

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 06-04-2019 kampuni ya **HIGHLAND ESTATES LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea MBARALI** kupitia MAKAMBAKO, gari hilo lenye namba za usajili:
   1. **T 935 DBQ / T 476 CBG**
   2. **T 919 DBQ / T 872 CDS**
3. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 20.00**
   **Upana - mita 3.20**
   **Kimo - mita 5.40**

   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215162302

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 06-04-2019 kampuni ya **F.M CARGO LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea KASUMULU** kupitia VIGWAZA, gari hilo lenye namba za usajili: T 269 CPW / T 597 DEA
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 20.00**
   **Upana - mita 4.20**
   **Kimo - mita 4.80**

   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215162602

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 06-04-2019 kampuni ya **BUSINESS TRUST TANZANIA LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea MTWARA** kupitia **NANGURUKURU,** gari hilo lenye namba za usajili:
   1. T 212 CAJ / T 560 ANP
   2. T 122 DGA / T 143 CBY
   3. T 908 DGB / T 788 DKM
4. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 18.00**
   **Upana - mita 2.70**
   **Kimo - mita 5.00**

   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215162502


KWA MATANGAZO

MADOGO MADOGO

TUPIGIE

***0767 223311***

***Kwa Habari Motomoto usikose***

***Gazeti lako la Nipashe kila siku***

***Tupigie 0767 223 311***


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# HAZARD AMPA DARASA HUDSON-ODOI CHELSEA

**LONDON, England**

EDEN Hazard hataraji Callum Hudson-Odoi kuwa na wakati mgumu wa kubaki mnyenyekevu kwa sababu ya wachezaji wenzake wanaomzungumza Chelsea.

Hudson-Odoi, ambaye alisajiliwa kutoka Bayern Munich Januari, alicheza mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu kwa Blues Jumatano.

Na katika mwanzo wake wa kwanza kwenye ligi akiwa na umri wa miaka 18, alitengeneza bao moja kwenye ushindi wa 3-0 dhidi ya Brighton and Hove Albion.

Hazard, ambaye alitamba Lille kabla ya kutua Chelsea, anaamini katika vyumba vya kubadilishia nguo ndani ya Stamford Bridge kuna chachu kubwa kwa Hudson-Odoi kubakia hapo.

"Nafikiri ni rahisi kwa sababu wachezaji wanaozungumza yeye ni wanyenyekevu," alisema Hazard.

"Kama tulikuwa tunafikiri kwamba sisi ndio bora, kwake yeye itakuwa ni ngumu kuwa mnyenyekevu. Lakini tuna akili na ana familia inayomjali.

"Nilimuambia kitu cha kwanza ni kubakia kuwa mnyenyekevu, afanye kazi kwa kujituma na kufanya mazoezi kwa nguvu, kufunga mabao, halafu atakuwa na furaha akiwa uwanjani. Anaweza kufika mbali."




# RAMSEY, KOSCIELNY, XHAKA SHAKANI KUIKOSA EVERTON

**LONDON, England**

Arsenal inasubiri kuchunguza kwanza kuwa fiti kwa Laurent Koscielny, Aaron Ramsey na Granit Xhaka kuelekea mechi yao ya kesho ya Ligi Kuu dhidi ya Everton.

'The Gunners' waliwakosa Xhaka na nahodha Koscielny wakati wakishinda 2-0 Jumatatu dhidi ya Newcastle United, matokeo ambayo yaliwafanya kucheza mechi sita mfululizo bila kupoteza kwenye ligi na kuingia ndani ya nne bora ya msimamo wa ligi hiyo.

Xhaka anauguza majeraha ya nyonga aliyoyapata wakati akiwa katika majukumu ya kimataifa na Uswisi, wakati Koscielny ni mchezaji mwingine ambaye hajacheza tangu waliposhinda kwenye mechi ya Europa League dhidi ya Rennes Machi 14, mwaka huu kwa sababu ya majeraha ya mguu. Arsenal pia inakabiliwa na hofu ya kumsubiri Ramsey, ambaye alitoka uwanjani dakika ya 67 wakati wa mechi dhidi ya Newcastle kutokana na majeraha ya nyonga, katika mchezo ambao alifunga bao la kwanza.

Hata hivyo, Unai Emery ana matumaini ya kuwatumia wote watatu kuelekea mechi hiyo ya kesho katika Uwanja wa Goodison Park katika kikosi chake cha Arsenal ambacho kitashuka uwanjani bila Lucas Torreira kutokana na kuwa nje akitumikia adhabu ya kadi nyekundu aliyoipata mwezi uliopita dhidi ya Tottenham.

Hector Bellerin, Rob Holding (wote majeraha ya goti) na Danny Welbeck (kifundo cha mguu) waliokosekana kwa muda mrefu hakuna uwezekano wakuwatumia msimu huu tena, ingawa Welbeck amerejea mazoezini.

# Klopp: Man City kama bora duniani

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesema kwamba, wapinzani wa Liverpool kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, Manchester City wanaweza kushinda mataji manne, akiongeza vijana hao wa Pep Guardiola kama timu bora duniani.

City walirudi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, ikiongoza kwa pointi moja dhidi ya Liverpool, shukrani kwa ushindi wa 2-0 dhidi ya Cardiff City.

Tangu kipigo cha kushitukiza cha 2-1 kutoka kwa Newcastle United mwishoni mwa Januari, City ilibadilisha gia na kushinda mechi nane



mfululizo za Ligi Kuu.

Kikosi cha Guardiola pia kimeshinda taji la EFL, ikiifunga Wembley kwa changamoto ya penalti, kikichukua hatua kuelekea kwenye nafasi ya kutwaa mataji manne.

Na ingawa kikosi cha Klopp kipo kwenye mbio moja na wapizani wao hao, wana nafasi pia kubwa ya kulitwaa taji hilo msimu huu.

"Kama tungekuwa tuangalia kutoka nje, unaweza kuangalia City wanaonekana kushinda kila kitu, yaani wana uwezo wa kushinda mataji manne," alisema Klopp kabla ya mchezo wa jana Ijumaa dhidi ya Southampton.

## HABARI MICHEZO



# DE BRUYNE

## AIPA ENGLAND NAFASI UBINGWA EURO 2020

**MANCHESTER, England**

ENGLAND wana nafasi ya kushinda Euro 2020 pamoja na Ufaransa, kwa mujibu wa kiungo wa Manchester City, Kevin De Bruyne.

Kikosi hicho cha Gareth Southgate kimejivuta hadi nafasi ya nne kwenye orodha ya viwango vya ubora vya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), baada ya mechi mbili za kufuzu Machi mwaka huu.

'Simba Watatu' hao walifuzu kutinga nusu fainali ya Kombe la Dunia mwaka jana kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990.

Na De Bruyne ambaye alifunga bao la pili la dakika za majeruhi katika ushindi wa City wa mabao 2-0 dhidi ya Cardiff City Jumatatu anaamini kikosi hicho kiko imara zaidi kushinda masindano hayo.

"Nimewaambia watu wa England wiki moja iliyopita kwamba wanatakiwa kushinda Euro 2020. Nafikiri wao wana nafasi kubwa pamoja na Ufaransa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nawaona England kwenye nafasi kubwa mno katika siku za usoni, naamini watafanya vizuri.

"Watashinda na kama wakishinda watakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi na nina imani kubwa watafanya hivyo kwa kipindi cha miaka 10 ijayo."

## Madrid wajipanga kumbakiza Varane

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid imeamua kutomuachia beki wake raia wa Ufaransa, Raphael Varane, huku taarifa zaidi zikidai kwamba watampa ofa ya ziada ya euro milioni tatu kila mwaka ili kumbakiza hapo Bernabeu.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 25, yeye mwenyewe anapigania kuondoka klabuni hapo wakati wa kipindi cha majira ya joto, akiwa ameshinda kila kitu kwa kipindi chake cha miaka nane aliyokaa hapo Madrid.

Alikuwa sehemu ya kikosi kilichoshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo, na sasa atataka kuondoka hapo Madrid huku kocha mpya Zinedine Zidane akitaka kumbakiza.

Gazeti la AS, limedai kwamba mshahara wake utapanda kutoka euro milioni sita hadi euro milioni tisa kama atakubali kubakia hapo.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022, lakini sasa klabu hiyo inataka kumbakiza nyota huyo kwa muda mrefu kwenye klabuni hiyo.

Zidane , ambaye ndiye aliyeshauri Varane kusajiliwa kutoka RC Lens mwaka 2011, kuna uwezekano mkubwa wa kuendelea kubakia na mabingwa hao wa Ulaya.

Hata hivyo, Klabu ya Paris Saint-Germain ndio timu inayoongoza kwenye mbio za kuwania saini yake, na pia Juventus wakimtaka kusajili ili kumrithi Leonardo Bonucci na Giorgio Chiellini.

Manchester United na Bayern pia zinawania saini yake.

## Spurs yavunja rekodi ya dunia kwa faida



**LONDON, England**

KLABU ya Tottenham Hotspur imejiwekea rekodi ya dunia ya pauni milioni 113 baada ya kukatwa kodi msimu uliopita. Fedha hizo zimeshinda faida ya paundi milioni 106 ilizopata Liverpool mapema mwaka huu.

Matokeo ya kila mwaka ya kifedha ya msimu wa 2017-18, yanaonyesha mapato ya Spurs yalipanda kutoka pauni milioni 310 hadi pauni milioni 380 kutokana na mauzo ya wachezaji, mashabiki wengi waliojitokeza katika Uwanja wa Wembley na kufuzu hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Takwimu hizo zimetolewa wakati ambapo klabu hiyo ilikuwa ikifungua uwanja wake mpya wa pauni bilioni moja, huku gharama hiyo ikiwa ilifikiwa kupitia mikopo.

Mapato yake katika Ligi Kuu ya England yameongezeka maradufu kutoka pauni milioni 19 hadi pauni 42.6 kufuatia ongezeko la mashabiki katika Uwanja wa Wembley.

Tottenham iliishinda Crystal Palace 2-0 katika uwanja wao mpya juzi.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# 'POGBA KAMA AKITAKA AONDOKE TU MAN UTD'

●●● Sasa ataka kulipwa pauni 500,000 kwa wiki ili kubaki Old Trafford...

**Manchester, England**

PAUL Pogba anapaswa kuondoka Manchester United kama hataki tena kuichezea klabu hii, amesema kiungo wa zamani wa 'Mashetani Wekundu' hao, Jesper Olsen.

Pogba amekuwa akihusishwa na kujiunga na Real Madrid mwishoni mwa msimu na kiungo huyo Mfaransa amesena 'Los Blancos' ni "klabu ya ndoto kwa kila mchezaji".

Kujiunga na Madrid kutamuwezesha Pogba kumuunganisha na raia mwenza Zinedine Zidane, ambaye ameripotiwa kupewa bajeti kubwa ya kukisuka upya kikosi chake.

Mustakabali wa baadaye wa Pogba hapo Old Trafford ulikuwa mashakani chini ya Jose Mourinho, lakini tangu Mreno huyo alipoondoka Desemba mwaka jana amekuwa tishio chini ya Ole Gunnar Solskjaer.

Tetesi mpya za kuondoka zimekuwa zikiendelea kujitokeza, na Pogba tayari alishawahi kuondoka United mara moja katika wasifu wake kisoka na kujiunga na Juventus, wakati aliposhindwa kuchomoza kikosi cha kwanza chini ya Alex Ferguson.

"Nadhani siku zilizopita Ferguson alikuwa sawa," Olsen aliiambia Omnisport.

"Kama hutaki kuichezea klabu hutakiwi kubaki! Na nadhani hilo ni suala pia kwa Pogba.

"Bila shaka unapaswa kuendelea bila yeye, lakini itakuwa vizuri kumuona akibaki pia, kwa sababu ni sehemu muhimu kwa timu."

Gazeti la The Sun, jana liliripoti kuwa Pogba, 26, ambaye ameendelea kuhusiswa na kujiunga na Real Madrid, anataka kulipwa pauni 500,000 kwa wiki ili kubaki Old Trafford.

Kama ilivyo kwa Pogba, Christian Eriksen amekuwa pia akihusishwa na kujiunga na Madrid mwishoni mwa msimu, wakati mkataba wake na Tottenham utakapokuwa umebakiza mwaka mmoja kumalizika.

Eriksen alitimiza mechi yake ya 200 kuichezea Spurs kwenye Ligi Kuu ya EPL wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Crystal Palace Jumatano, mchezo ambao ulikuwa wa kwanza kwao kucheza katika uwanja mpya wa Tottenham Hotspur.

Nyota wa zamani wa kimataifa wa Denmark, Olsen anaona kuwa Eriksen pengine anataka kujaribu mwenyewe katika ligi mpya, wakati huu kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27 kwa sasa akiwa kwenye kiwango cha juu katika wasifu wake kisoka.

"Ni muhimu, bila shaka, si mchezaji mbinafsi pia," Olsen aliongeza kuhusu raia mwenza huyo, ambaye pia amekuwa akihusishwa na kujiunga na vinara wa La Liga, Barcelona.

"Ana ubora wa hali ya juu, mara nyingine anaweza kufanya zaidi ya anachokifanya kwa sababu ni mchezaji asiye na ubinafsi ambaye hujui mara nyingi, lakini ni kiunganishi kikubwa cha Tottenham. Ubora wa hali ya juu, hakuna hofu kuhusu hili.

"[Kutua La Liga kujiunga na Madrid ama Barca] kunaweza kuwa changamoto kubwa kwake kwa uhakika. Amekuwapo England kwa kipindi kirefu. Ajax na kisha Uingereza, kama Wadenmark tunapenda kujaribu sehemu mbalimbali na kuzoea vitu tofauti, hivyo nadhani huo utakuwa uzoefu mkubwa kwake pia."

## KWA UFUPI

**ARSENAL YAMPAGAWISHA FRASER**

WINGA wa Bournemouth na Scotland, Ryan Fraser 25, amesema amepagawa kuhusishwa na kujiunga na Arsenal. ***(Sky Sports)***

**MADRID YAMTENGEA DAU BAILLY**

Real Madrid inataka kumnunua beki wa kati wa Manchester United na Ivory Coast, Eric Bailly, 24, kwa pauni milioni 35 majira haya ya joto. ***(Sun)***

**RICHARLISON KUTIMKIA LIVERPOOL**

STRAIKA wa Everton, Mbrazil Richarlison, 21, anaweza kuwa akijiandaa kujiunga na majirani wao, Liverpool. ***(Esporte via ESPN)***

**PSG YAMKUBALIA DE GEA**

Paris St-Germain ipo tayari kufikia dau la mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki anazozitaka kipa wa Manchester United na Hispania, David de Gea, 28, endapo atakubali kujiunga na miamba hiyo ya Ufaransa. ***(Independent)***

**SOLSKJAER AKUNWA NA WAINGEREZA**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, angependa kununua zaidi wachezaji wa Kiingereza na anavutiwa na nyota wawili wa kimataifa wa England, Kiungo wa West Ham, Declan Rice, 20, na winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, 18 pamoja na beki wa kulia wa Crystal Palace na England U-21, Aaron Wan-Bissaka, 21. ***(Times)***

**BENITEZ ATAFUTA KAZI UFARANSA**

KOCHA wa Newcastle, Rafael Benitez, amewataka mawakala wake kumtafutia kazi katika klabu za Ligi Kuu Ufaransa. ***(L'Equipe, via Chronicle)***

**SANCHO APIGIWA HESABU UTD**

Manchester United inavutiwa na dila la pauni milioni 100 la kumsajili winga wa England na Borussia Dortmund, Jadon Sancho, 19. ***(Independent)***

**WARNOCK KUITEMA CARDIFF**

KOCHA wa Cardiff, Neil Warnock, anapanga kuachana na klabu hiyo hata kama wataepuka kushuka daraja kutoka Ligi Kuu. ***(Sun)***

**TIELEMANS ANOGEWA LEICESTER**

KIUNGO Mbelgiji Youri Tielemans, 21, anatumai kuongeza mkataba wake wa mkopo wa miezi sita na Leicester akitokea Monaco. ***(Sky Sports)***

**SESSEGNON KUONDOKA FULHAM**

Fulham imenyoosha mikono juu kumpoteza nyota wa kimataifa wa England U-21, Ryan Sessegnon, 18, ambaye anaweza kucheza beki wa kushoto ama winga wa kushoto, baada ya kushindwa kujinusuru kubaki Ligi Kuu. ***(Standard)***

**DEFOE HATAONDOKA RANGERS**

STRAIKA Jermain Defoe 36, amesema atabaki Rangers kwa msimu ujao na hatakatisha mkataba wake wa miezi 18 wa mkopo kutoka Bournemouth . ***(Daily Record)***

**SHERWOOD KUMRITHI MCCLAREN**

KLABU ya Queens Park Rangers imemuweka kocha wa zamani wa Tottenham na Aston Villa, Tim Sherwood kama chaguo lao la kwanza katika kurithi mikoba ya kocha Steve McClaren. ***(Standard)***



HABARI MICHEZO

# KOCHA SERENGETI ABAINI KITU WAKITWAA UBINGWA

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kutwaa ubingwa wa mashindano maalumu ya vijana ya umri chini ya miaka 17 yaliyomalizika juzi jijini Kigali, Rwanda, Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Oscar Milambo, amesema kuwa bado anahitaji kuimarisha safu yake ya ulinzi.

Serengeti Boys juzi ilitwaa ubingwa wa mashindano hayo yaliyoshirikisha nchi tatu, lakini ikitoka sare ya mabao 3-3 na yosso wenzao wa Rwanda ikiwa ni baada ya awali kuichapa Cameroon 2-1.

Milambo alisema kuwa kuruhusu mabao matatu si jambo zuri, hivyo watayafanyia kazi makosa yaliyojitokeza kwa lengo la kujiimarisha na hatimaye kuwa imara kabla ya kuanza kwa fainali za Afrika za Afcon U-17 baadaye mwezi huu.

"Tunamshukuru Mungu kwa kufanya vizuri katika mashindano haya, lakini nimeona safu yangu ya ulinzi haikufanya kile tulichokitarajia, kukubali kufungwa mabao matatu katika mechi moja ni hatari, tutatumia hizi siku 10 zilizobaki kujirekebisha," alisema kocha huyo.

Naye Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, aliwapongeza yosso hao kwa mafanikio waliyopata katika michuano hiyo na kuwataka Watanzania waendelee kusubiri kupokea vikombe vingi zaidi.

Karia alisema michuano hiyo imeendelea kuwaimarisha Serengeti Boys ambao watakuwa wenyeji wa fainali za Afrika za Vijana za mwaka huu.

Fainali hizo za AFCON U17 zitaanza Aprili 14 hadi 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa, Uhuru na Azam Complex, vyote vya jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (kulia), akipozi katika picha na Waziri wa Utalii na Maliasili, Hamisi Kigwangala (kushoto), baada ya Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abbas (katikati), kumkabidhi Mwakyembe Cheti cha Shukrani kwa wizara yake kufuatia ushiriki wao na kufanikisha michuano ya SportPesa Cup 2019 iliyofanyika nchini Februari mwaka huu na kuchangia kuitangaza Tanzania kimichezo na utalii barani Afrika. Makabidhiano hayo yalifanyika Ofisi ndogo ya Wizara ya Michezo Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SPORTPESA**

# Matola: Hofu kuimaliza Yanga FA

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA mchezo wa hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Lipuli FC, Selemani Matola, amesema hali ya hofu na wasiwasi ni moja ya sababu ambazo zinaweza kuwaangusha wapinzani wao, Yanga.

Lipuli FC itaikaribisha Yanga katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA ambayo itachezwa mwishoni mwa mwezi huu kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matola alisema matokeo ya ushindi anayopata katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazoendelea yanakiimarisha zaidi kikosi chake na kuongeza morali.

Matola alisema anakiamini kikosi chake na wamejipanga kufanya vema katika mechi hiyo ili waweze kutinga fainali na hatimaye kuibuka mabingwa wa michuano hiyo kwa mara ya kwanza.

"Sisi tunaendelea kujiimarisha, ila kwa hali ya kawaida, Yanga ndio wenye hofu ukilinganisha na sisi, na hali hiyo wakiiruhusu, itawamaliza," alisema kwa kifupi kocha huyo na nahodha wa zamani wa Simba.

Aliongeza kuwa anataka kuweka rekodi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika mwakani akiwa na klabu hiyo na anaamini uwezo wa kushinda taji hilo wanao.

Lipuli walitinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo baada ya kuifunga Singida United mabao 2-0 wakati Yanga iliwatoa Alliance FC kwa penalti 4-3 baada ya kutoka sare ya bao 1-1 katika dakika 90 za kawaida.

Mtibwa Sugar ya Morogoro ndio walikuwa mabingwa watetezi wa mashindano hayo, lakini waliliachia kombe hilo baada ya kuiaga mapema michuano hiyo ambayo inachezwa kwa mfumo wa mtoano.

# Bunge lakataa kuichangia Yanga

INATOKA UK . 32

Baada ya wabunge kuhojiwa, Naibu Spika alisema wabunge waliopinga kuichangia Yanga wameshinda, hivyo Bunge halitakata posho za wabunge kwa lengo la kupata fedha za kuisaidia timu hiyo.

Hali ya kiuchumi ya klabu hiyo iliyoanzishwa mwaka 1935, imeendelea kuwa mbaya kutokana na kujiuzulu kwa uongozi na kutokuwa na mfumo imara wa vyanzo vya mapato na ukusanyaji wa fedha kutoka kwa wananchama.

Kutokana na ukata huo, uendeshaji wa klabu hiyo umekuwa mgumu, mara kadhaa ikiripotiwa wachezaji wake kushindwa kulipwa mishahara huku kocha mkuu Mwinyi Zahera akidaiwa kuweka bayana kuwa hataendelea kuitumikia kama itashindwa kukusanya Sh. bilioni moja zitakazotumika kwenye usajili wa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

# Mabao 11 yaiponza Ujamaa 6-bora Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya kusimamia mashindano na Ligi ya Chama cha Soka Zanzibar (ZFA), imeiondoa Klabu ya Ujamaa katika orodha ya timu sita zilizotinga hatua ya sita-bora ya Ligi Daraja la Pili Taifa, kusaka kupanda Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja baada ya kubainika kupanga matokeo katika mechi yao ya mwisho.

Timu ya Ujamaa ambayo ina historia kubwa katika medali ya soka visiwani hapa kutokana na viongozi wengi wa serikali kuichezea kwa nyakati tofauti wakiwamo wachezaji wengi maarufu, imefungiwa kutokana na ushindi wake wa mabao 11-0 ilioupata Machi 18, mwaka huu dhidi ya White Bird.

Katika mechi hiyo, Ujamaa ilishuka dimbani ikiwa inahitaji ushindi wa kuanzia mabao 9-0 ili iweze kucheza sita- bora, hivyo ikashinda 11-0, hatua ambayo Kamati ya Mashindano ya ZFA katika uchunguzi wake imejiridhisha kuwapo kwa upangaji wa matokeo.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa kamati hiyo, Hussein Ahmada, alisema kitendo hicho hakivumiliki na wamechukuwa uamuzi wa kufuta mchezo huo na badala yake nafasi hiyo wameitoa kwa timu ya Mfenesini.

Alisema kamati ilikaa kikao juzi na kupitia ripoti za mchezo huo zilizotumwa na waamuzi, kamishna wa mchezo na waangalizi na kugundua kuwa katika mechi hiyo kulikuwapo na rushwa na upangaji wa matokeo wa waziwazi.

Alifafanua kuwa mbali ya kupitia ripoti hizo tatu, lakini pia waliwaita baadhi ya viongozi wa pande zote mbili na kuwahoji ambapo walishindwa kujibu baadhi ya maswali. "Tuliwaita viongozi wa timu zote mbili na kuwahoji kwa nyakati tofauti baada ya mahojiano kuna baadhi ya maswali walishindwa kuyajibu kwa ufasaha kitu ambacho kilitupa mashaka na kamati kubaini hayo ambayo tuliyapata," alisema.

Alisema maamuzi hayo waliyoyatoa ni kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha kanuni ya kuendesha mashindano na ligi ya chama hicho. Aidha, alisema kamati yao ipo makini sana katika kufuatilia michezo hasa ile ambayo hutoa nafasi kwa timu moja kupanda ama kushuka daraja ili kuhakikisha haki inatendeka kwa pande zote mbili.

Kwa mujibu wa kanuni, mashindano hayo ya Ligi Daraja la Pili Taifa, yaligawanywa katika makundi matatu ambapo kila kundi lilitakiwa kutoa timu mbili zitakazoshika nafasi ya kwanza na ya pili kutinga hatua ya sita bora, hivyo kutokana na uamuzi huo timu zilizotinga hatua hiyo kutoka Kundi C sasa ni Dula Boys na Mfenesini.

# Michezo

Jumamosi Aprili 6, 2019

Nipashe




## ‘Pogba kama akitaka aondoke tu Man Utd’

HABARI UK 30

**KAZI IMEANZA...**




Wachezaji wa Serengeti Boys wakifurajia  Kombe na Medali zao juzi baada ya kukabidhiwa kufuatia kuibuka mshindi wa jumla wa michuano maalum ya kujiandaa na fainali za Afcon U-17 iliyofanyika mjini Kigali, Rwanda. Serengeti Boys ambao watakuwa wenyeji wa fainali za Afcon U-17, zitakazofanyika Aprili 14-28, mwaka huu, katika michuano hiyo iliichapa Cameroon mabao 2-1 na kisha kutoka sare ya 3-3 na wenyeji, Rwanda. **HABARI UK. 31**

# SIMBA: NI USHINDI TU

## ●●● Aussems ataka matatu ya mapema, Mo awaita mashabiki, TP Mazembe wagwaya, waonya...

**Na Somoe Ng’itu**

‘YES we can’ ndiyo kauli mbiu inayoendelea kutumika wakati Simba ikitarajia kuwakaribisha TP Mazembe kutoka Kongo (DRC), katika mchezo wa kwanza wa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika mkutano wa waandishi wa habari jana, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, alisema kuwa vijana wake wako tayari kwa mechi hiyo na wamejiandaa kucheza kwa mfumo wa kushambulia kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mchezo.

Aussems alisema kwamba anaamini mfumo huo utamsaidia kuibuka na ushindi na kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele na kuufanya mchezo wa marudiano utakaochezwa Aprili 12, mwaka huu mjini Lubumbashi kuwa mwepesi kwao.

Mbelgiji huyo alisema pia wachezaji wake wote wako katika hali nzuri, morali ya juu na wamejiandaa kuendeleza ushindi ili kuwapa furaha mashabiki wao.

Hata hivyo, Aussems alisema anafahamu mechi hiyo inatarajiwa kuwa ngumu, lakini hatakuwa na sababu ya kubadilisha mfumo wa kucheza, na wamejiandaa kucheza kwa kushambulia kama walivyofanya katika mechi zilizotangulia ambazo walipata ushindi wakiwa hapa nyumbani.

“Siwezi kubadilisha mfumo, tutaendelea kucheza kwa kushambulia kama tulivyocheza mechi za mwanzo, naamini hata tukifungwa bao moja na sisi kufunga mabao matatu halitakuwa jambo baya, kikubwa ni kupata ushindi, au tukifanikiwa kutoruhusu bao itakuwa vizuri sana kwetu,” alisema Aussems.

Aliongeza kuwa hata katika mechi ya marudiano ataendelea kucheza kwa kushambulia na anaamini mfumo huo utamweka salama zaidi kuliko ‘ kupaki basi’.

Nahodha wa TP Mazembe, Tressor Mputu, alisema amefurahi kurejea tena jijini hapa na anaamini timu yake itaondoka na ushindi katika mchezo huo.

“Tumekuja kushinda, hatukuja kutembea, tunajua Simba pia ni timu kubwa, lakini Mazembe iko juu zaidi, tutajipanga kuwazuia wachezaji wao wakali ili wasitupe tabu,” Mputu alisema.

**MO: MAZEMBE WANAFUNGIKA**

Mwekezaji wa Simba, Mohamed ‘MO’ Dewji amewataka mashabiki wa timu hiyo kuendelea kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu yao na kueleza kuwa TP Mazembe, mabingwa mara tano wa Ligi ya Mabingwa Afrika wanafungika. Mo alisema anakiamini kikosi chake kitaendelea kujitoa kama kilivyofanya katika mechi nyingine zilizotangulia katika mashindano hayo.

“Mashabiki wamekuwa na mchango mkubwa sana kwa timu, kama mlivyojilipua katika mechi iliyopita (dhidi ya Al Ahly), nawaomba mjitokeze kwa wingi kuishangilia timu yetu, wanaongeza hamasa kwa wachezaji, na sehemu kubwa ya fedha zinazopatikana zinatumika katika kuwapa motisha,” alisema Mo.

Kuhusu hatima ya wachezaji, Meddie Kagere na Clatous Chama ambao wanawindwa na klabu nyingine, Mo alisema itakuwa kazi ngumu kuwaruhusu nyota hao kwa sababu anaamini bado kocha anawahitaji.

“Bado wana mikataba, kama ni kuuzwa, basi watauzwa kwa gharama kubwa, kwa sababu sisi tunahitaji ushindi zaidi kuliko pesa,” alisema mfanyabiashara huyo.

Aliongeza kwa kuzitaka klabu tajiri kujiandaa kupambana na Simba katika dirisha la usajili kwa sababu mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wamejipanga kusajili wachezaji nyota ili kuimarisha kikosi chao.

# Bunge lakataa kuichangia Yanga

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

WABUNGE wamekataa kukatwa posho zao ili kuichangia Klabu ya Yanga ambayo inakabiliwa na hali ngumu ya kiuchumi.

Wakati watunga sheria hao walikataa posho zao kukatwa kuichangia Yanga, Mbunge wa Nkasi, Ally Kessy  (CCM), ameiomba serikali iingize klabu hiyo ya Jangwani kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (Tasaf).

Mara tu baada ya kumalizika kwa kipindi cha ‘Maswali’ bungeni mjini Dodoma jana, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliwatambulisha wajumbe wa kamati ya hamasa ya kuchangia Yanga na kusababisha baadhi ya wabunge kupiga makofi huku wengine wakidai wajumbe wa kamati hiyo ni “ombaomba”.

Baada ya utambulisho huo huku kelele zikiendelea kutawala ndani ya Ukumbi wa Bunge, Mbunge wa Nkasi, Kessy alisimama na kuomba mwongozo kwa Naibu Spika.

“Mheshimiwa Naibu Spika; kwa kuwa Kamati ya Yanga imefika kuomba mchango, naomba kipitishwe kikapu, akabidhiwe (Venance) Mwamoto (Mbunge wa Kilolo - CCM) au (George) Mkuchika (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) wakusanye fedha au naomba serikali iiweke timu hiyo kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini,” Kessy alisema na kuibua vicheko na shangwe bungeni.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, Dk. Tulia alisema anaona ni vyema Kessy akubaliwe mwongozo wake kwa wabunge kukatwa posho ili kuichangia timu hiyo.

Kauli hiyo ya Naibu Spika iliibua shangwe kwa wabunge walioonekana kuwa wapenzi wa Yanga, lakini ilipingwa vikali na baadhi ya wabunge ambao hawakuwa tayari kukatwa posho zao.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Spika aliamua kutolea mwongozo suala hilo akisema: “Kwa sababu mwongozo huo ni jambo ambalo linahusu wabunge kuridhia, nitawahoji, wale wanaoridhia waseme ndiyo na wanaopinga waseme siyo,” Dk. Tulia aliagiza.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >